# Nipashe

Jumamosi Agosti 22, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580317

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wasichana wazidi kuwaburuza wavulana mtihani kidato cha 6

UKURASA 4




UKURASA 11

# Waliokatwa wafunguka

**WENGI** wakubali yaishe, Profesa achambua uteuzi wagombea ubunge CCM... *Endelea uk. 3*



Andrew Chenge.




Paul Makonda.

# PATACHIMBIKA MAJIMBONI

UKURASA 2

### ARUSHA MJINI



Mrisho Gambo - CCM



Godbless Lema- Chadema

### KIGOMA MJINI



Kilumbe Ng'enda-CCM



Zitto Kabwe-ACT-Wazalendo

### TARIME VIJIJINI



Mwita Waitara - CCM



John Heche - Chadema

### IRINGA MJINI



Msambatavangu - CCM



Peter Msigwa-Chadema

### MBEYA MJINI



Dk. Tulia Ackson - CCM



Joseph Mbilinyi - Chadema

### VUNJO



Dk. Charles Kimei-CCM



James Mbatia-NCCR- Mageuzi

### KAWE



Askofu Gwajima-CCM



Halima Mdee-Chadema

### SAME MASHARIKI



Anne Kilango - CCM



Naghenjwa Kaboyoka-Chadema

### HAI



Saashisha Mafuwe - CCM



Freeman Mbowe - Chadema

**MICHEZO** MUGALU HESABU KALI KWA BOCCO, KAGERE UK.23

**MAONI, KATUNI UK.6**


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipokea fomu ya kugombea ubunge Jimbo la Ruangwa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi na Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ruangwa, Frank Chonya, jana. **PICHA: OWM**

# Patachimbika majimboni

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), juzi kilipitisha majina ya wanachama 264 kugombea ubunge katika majimbo katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Katika orodha ya wanachama hao, wamo waliokuwa mawaziri, makatibu wakuu, wakuu wa mikoa na wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na watu mashuhuri kwenye fani na tasnia mbalimbali.

Kupitishwa kwa wanachama hao, kumetoa picha halisi ya ushindani katika majimbo mbalimbali, huku wengine wakionekana kupata unafuu kutokana na hali ya kisiasa katika maeneo yao. Mvutano huo pia unatokana na uwezo na mizizi ya kisiasa katika maeneo husika.

Baadhi ya wanasiasa walioteuliwa katika kuwania ubunge ambao watakuwa na mchuano mkali ni kama wafuatao;-

**MDEE NA GWAJIMA**

Jimbo la Kawe linatarajiwa kuwa na mnyukano mkali kati ya kiongozi wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, atakayepambana na Halima Mdee wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Wawili hao wanatarajia kupambana vikali, kwanza, umaarufu wa kila mmoja. Mdee amejijengea umaarufu mkubwa katika medani ya siasa tangu alipochomoza miaka 15 iliyopita akianzia ubunge wa viti maalum mwaka 2005 kabla ya kuwania jimbo hilo mwaka 2010 na kuibuka na ushindi mara mbili mfululizo.

Gwajima, ambaye ana wafuasi wengi katika kanisa lake, amekuwa maarufu katika miaka ya karibuni kutokana na kuwashambulia hadharani watu mashuhuri na kutoa kauli ambazo zimekuwa zikivuta hisia kali.

Kiongozi huyo wa kiroho, ameteuliwa kugombea ubunge Kawe licha ya kushika nafasi ya tatu katika kura za maoni kwa kupata kura 71 nyuma ya Furaha Dominic aliyepata kura 101 na Angela Kizigha (85).

**SUGU NA DK. TULIA**

Mnyukano mwingine utakuwa kati ya msanii wa muziki wa Hip Hop, Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu, na Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwenye jimbo la Mbeya Mjini.

Sugu ambaye amekuwa mbunge katika jimbo hilo kwa miaka 10, anatarajiwa kupata upinzani mkali kutoka kwa Dk. Tulia anayewania nafasi hiyo kupitia CCM.

Wawili hao wamekuwa na vita vya baridi kisiasa na sababu kubwa imekuwa ubunge katika jimbo. Baada ya malumbano na kupigana vijembe, sasa watachuana rasmi kuwania jimbo hilo na mshindi atapatikana.

**MSIGWA NA MSAMBATAVANGU**

Mchungaji Peter Msigwa kapata au kapatikana? Hilo ni swali ambalo watu wanaofuatilia masuala ya siasa wanajaribu kujiuliza baada ya Jesca Msambatavangu kupitishwa na CCM kugombea ubunge katika jimbo la Iringa Mjini.

Mwanamama huyo ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa kabla ya kufukuzwa uanachama na kisha kurejeshwa, anaonekana ndiye turufu ya kulirejesha jimbo baada ya kulipoteza kwa miaka 10.

Kutokana na uteuzi huo, inabashiriwa kutakuwa na mchuano mkali. Hiyo inatokana na nguvu ya ushawishi kutoka kwa wanasiasa hao wawili na kuwa na wafuasi wengi kila mmoja.

Jambo lingine linaloonyesha kuwa kutakuwa na ushindani mkubwa ni ulinganisho wa wapinzani wa Msigwa mwaka 2010 na 2015 waliodaiwa kuwa hawakuna na nguvu dhidi yake. Lakini Msambatavangu kutokana na nguvu aliyonayo ndani ya Iringa, inaonyesha kuwa atamtoa jasho Msigwa katika mtanange huo.

**LEMA NA GAMBO**

Wanasiasa hao wanatabiriwa kuchuana vikali katika kupata ushindi jimbo la Arusha Mjini. Wote ni wazoefu katika jimbo hilo kutokana na kila mmoja kuliongoza kwa nafasi yake.

Lema amekuwa Mbunge wa Arusha Mjini kwa miaka 10 tangu mwaka 2010 wakati Gambo amekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwa miaka kadhaa na katika muda huo wamekuwa wakitifuana katika harakati za hapa na pale kisiasa.

Kuteuliwa kwa Gambo na kutokana na historia ya wawili hao katika ulingo wa siasa, inatabiriwa kwamba kutakuwa na ushindani mkali baina yao na kwamba mshindi hatapatikana kwa njia rahisi.

**HECHE NA WAITARA**

Baada ya kujiengua kutoka Ukonga, Naibu Waziri Ofisi ya Rais tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Mwita Waitara, alijaribu turufu yake Tarime Vijijini na ameteuliwa.

Kupata tiketi hiyo kunaonekana ni mkakati mzito wa CCM kulirejesha jimbo la Tarime Vijijini kutoka CHADEMA baada ya John Heche kushinda katika uchaguzi uliopita.

Heche na Waitara ni wanasiasa wanaofahamiana kwa muda mrefu, hivyo kuwapo kwao jimboni humo kunatarajiwa kuwapo upinzani mkali baina yao.

**ZITTO NA KILUMBE**

Mbunge machachari na Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, anagombea tena katika jimbo la Kigoma Mjini ambalo amekuwa akilishikilia tangu mwaka 2015. Kabla ya hapo, alikuwa mbunge wa Kigoma Kaskazini kwa miaka 10 tangu mwaka 2005 kupitia CHADEMA.

Katika uchaguzi uliopita, Zitto alimshinda Dk. Amani Kabourou, aliyekuwa mwanasiasa mkongwe na ambaye aliwahi kuwa mbunge wa jimbo hilo kupitia CHADEMA kabla ya kujiunga na CCM.

Safari hii, CCM imemteua Kilumbe Ng'enda, mwanasiasa asiyejulikana sana lakini ni mwenye mbinu mbalimbali katika medani ya kisiasa. Kuteuliwa kwake kunatarajia kuleta upinzani mkali kwenye kinyang'anyiro cha ubunge wa jimbo hilo.

**MBOWE NA MAFUE**

CCM katika uchaguzi wa mwaka huu, wamemteua Salashia Mafue kupambana na kisiki wa kisiasa, Freeman Mbowe katika kujaribu kulirejesha jimbo la Hai baada ya kulipoteza miaka 10 iliyopita.

Jimbo hilo kutokana na hali ya kisiasa ilivyo, linatarajiwa kuwa moja ya yale ambayo macho na masikio ya Watanzania, yatakuwa yakifuatilia kama CCM itafanikiwa kumng'oa Mbowe kutokana na mikakati iliyokuwa imewekwa kwa muda mrefu.

**MBATIA NA KIMEI**

Mchuano mwingine unatarajiwa kuwapo katika jimbo la Vunjo mkoani Kilimanjaro kati ya mwenyekiti wa NCCR- Mageuzi, James Mbatia na Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei.

Mbatia, ambaye alikuwa Mbunge katika jimbo hilo, anajaribu kutetea kurejea katika chombo hicho cha kutunga sheria lakini katika kuhakikisha inalirejesha baada ya kulipoteza kwa miaka 10, CCM imeamua kumteua Dk. Kimei katika mpambano huo.

**KABOYOKA NA KILANGO**

Naghenjwa Kaboyoka na Anne Kilango Malecela, wote walikuwa wabunge. Kaboyoka alikuwa mbunge wa Same Mashariki na aliyemwangusha Kilango aliyekuwa katika jimbo hilo tangu mwaka 2005.

Kutokana na wawili hao kuwapo katika orodha ya uteuzi kuwania jimbo hilo kupitia vyama vyao, historia ya ushindani baina yao inatarajiwa kurejea katika uchaguzi wa mwaka huu. Katika kinyany'anyiro hicho, Kaboyoka atakuwa akitaka kuendeleza ubabe wake ilhali Kilango akijaribu kulipiza kisasi cha kuangushwa mwaka 2015.

## Aliyepata kura 12 kwa wajumbe apeta uteuzi

**Na Waandishi Wetu**

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amepenya katika uteuzi wa wagombea ubunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), licha ya kuambulia kura 12 na kushika nafasi ya saba kwenye mchakato wa kura za maoni ndani ya chama.

Katika orodha ya wateule hao iliyotangazwa juzi jijini Dodoma na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, baada ya kumalizika kwa vikao vya juu vya chama, Katambi ameteuliwa kuwania ubunge wa Shinyanga Mjini. Wakati wa upigaji kura za maoni ndani ya CCM Jimbo la Shinyanga Mjini, Katambi alipata kura 12 na kushika nafasi ya saba, nyuma ya kinara Stephen Masele ambaye alikuwa akitetea kiti chake. Masele ambaye ameliongoza Bunge hilo kwa miaka 10, alipata kura 152, akifuatwa na Jonathan Ifunda aliyepigiwa kura 65 na Gasper Kileo aliyelamba kura 51.

**UCHUKUAJI FOMU**

Jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alikuwa miongoni mwa wateule wa CCM waliochukua fomu ya kugombea ubunge, akikabidhiwa na Frank Chonya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa liliko Jimbo la Ruangwa analowania tena.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, alichukua fomu kuwania ubunge kupitia CCM, huku akiahidi kuzingatia masharti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC), ikiwamo kufanya kampeni kistaarabu. Mavunde alichukua fomu jana katika Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, Wakili Msekeni Mkufya, akisema: "Hatuendi kutukana wala kusemana vibaya, wananchi hawataki matusi wala kauli zozote za kudhalilisha, wanataka kusikia kuhusu maendeleo."

Wagombea watatu pia walichukua fomu katika Jimbo la Kongwa ambao ni Emmanuel Ngobito (SAU), Bwabwio Mbahuka (ADC) na Edson Mbena (CHADEMA). Katika Jimbo la Bahi, mgombea wa CHADEMA, Amina Kanyama, alichukua fomu kuwania ubunge wa jimbo hilo sambamba na Meckzedecki Lesaka (NCCR Mageuzi), Mussa Malecela (UPDP) na Paschal Lwago (TADEA).

Jimbo la Chemba, waliokuwa wamechukua fomu hadi jana ni Mohamed Monni (CCM), Kunti Majala (CHADEMA) na Tanzilu Isema(CUF).

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, pia alichukua fomu ya kuwania ubunge Vwawa mkoani Songwe. Alikabidhiwa fomu hiyo jana na Msimamizi wa Uchaguzi Wilaya ya Mbozi, Hanji Godigodi.

Vilevile, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alichukua fomu ya kugombea ubunge Karagwe, huku Seif Gulamali akichukua fomu ya kuwania tena ubunge wa Jimbo la Manonga wilayani Igunga mkoani Tabora.

# Waliokatwa CCM watoa ya moyoni

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutangaza majina ya wanachama wake walioteuliwa kupeperusha bendera kwenye kinyang'anyiro cha ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, vigogo waliokatwa wametoa ya moyoni kuhusu uamuzi uliofanywa dhidi yao.

Wakizungumza jana katika mahojiano maalum na Nipashe, baadhi ya wanachama hao ambao wengine walikuwa mawaziri na wabunge wazoefu, walisema wamekubaliana na uamuzi uliofanywa na vikao vya juu vya chama.

**ANDREW CHENGE**

Aliyekuwa Mbunge wa Bariadi mkoani Simiyu, Andrew Chenge, ambaye aliongoza kura za maoni katika jimbo hilo, alipoulizwa kuhusu uamuzi uliofanywa dhidi yake, alijibu kwa kifupi kwamba amefurahi sana. "Nimefurahi sana," alijibu Chenge ambaye amekuwa mbunge kwa kipindi kirefu na kutoa mchango mkubwa katika utungaji wa sheria na uandaaji wa bajeti ya serikali.

Nipashe pia iliuliza Chenge kama yuko tayari kushiriki kampeni kukisaidia chama kupata ushindi na akatoa jibu lilelile kwamba amefurahi sana.

**DK. HARRISON MWAKYEMBE**

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ambaye ameanguka katika kumsaka mgombea wa CCM Jimbo la Kyela mkoani Mbeya, alisema ameupokea uamuzi wa vikao vya juu vya chama kwa mikono miwili na atashirikiana na wateule kukiwezesha chama kupata ushindi.

"Ninayaheshimu maamuzi (uamuzi)ya chama. Kilichobaki ni kukisaidia ili wateule waweze kupata ushindi," alisema Dk. Mwakyembe ambaye katika kura za maoni alishika nafasi ya tatu.

**ADADI RAJABU**

Aliyekuwa Mbunge wa Muheza mkoani Tanga, Adadi Rajabu, pia alisema ameupokea kwa 'roho moja tu' uamuzi wa vikao vya juu vya CCM na kuahidi kushiriki kumpigia kampeni mgombea aliyepitishwa na chama hicho kuwania ubunge wa jimbo hilo.



Dr-Harrison-Mwakyembe



Charles Kitwanga

**PAUL MAKONDA**

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, pia alitumia ukurasa wake rasmi wa Instagram kutoa maoni yake kuhusu uteuzi huo akisema: "Ninamwabudu Mungu aliye hai, hata kama asipojibu sawa na maombi yangu, bado atabaki kuwa Mungu wangu."

Makonda alilazimika kupoteza cheo ya ukuu wa mkoa alipochukua fomu ya kuomba ridhaa ya CCM kuwania ubunge wa Kigamboni jijini Dar es Salaam, ambako alishika nafasi ya pili kwenye kura za maoni ndani ya chama hicho nyuma ya kinara Dk. Faustine Ndugulile ambaye pia ameteuliwa na vikao vya juu vya chama.

**CHARLES KITWANGA**

Aliyekuwa Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga, alisema aliyeteuliwa na chama ni uamuzi wa Mungu na hivyo hana sababu ya kupinga uamuzi uliotolewa na vikao vya juu vya chama.

"Ninampenda mwenyezi Mungu, ninampenda Rais wangu, ninakipenda chama changu. Nitashiriki kampeni kama kawaida, mimi ni mtu wa Mungu, siwezi kumkosea Mungu, akitoka Mungu juu duniani, anakuja Rais, hakuna mwingine. Sasa kama ninampenda Mungu, nitashindwaje kumpenda Rais?" alihoji.

Kitwanga alisema Rais John Magufuli ni rafiki yake wa siku nyingi, hivyo anaamini kila anachokifanya ni kwa nia njema na yeyote atakayezungumza kinyume chake, atakuwa anamkosea Mungu.

**MARY CHATANDA**

Mary Chatanda, aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Mjini mkoani Tanga, alisema amepokea vizuri uamuzi wa chama kwa sababu ni utaratibu wa chama kila inapotokea kipindi cha uchaguzi, wanachama wanajitokeza wengi kugombea na mwisho anateuliwa mmoja.

**FURAHA DOMINICK**

Kama ilivyokuwa kwa wenzake, Furaha Dominick, aliyeongoza kura za maoni ndani ya chama kumsaka mgombea wa CCM Jimbo la Kawe, alisema amekubaliana na uamuzi wa vikao vya juu vya chama kumteua Askofu Josephat Gwajima kupeperusha bendera yao.

Alisema atamuunga mkono Askofu Gwajima na watatumia mbinu za vijana kumng'oa Halima Mdee anayewania tena ubunge wa jimbo hilo kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Askofu Gwajima alishika nafasi ya pili kwenye kura za maoni ndani ya CCM kumsaka mgombea wa jimbo hilo.

■ **Imeandikwa na Thobias Mwanakatwe na Mary Geofrey**

# Profesa auchambua uteuzi wa CCM

**Na Mary Geofrey**

PROFESA Gaudence Mpangala, mtaalam wa Sayansi ya Siasa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), amechambua uteuzi wa wagombea ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Katika mazungumzo mahususi na Nipashe kuhusu uteuzi huo jana, Profesa Mpangala alisema anaona kuna ukakasi katika kukatwa kwa majina ya wagombea waliokuwa wameongoza kwenye mchakato wa kura za maoni ndani ya chama.

Juzi, Halmashauri Kuu wa CCM Taifa (NEC), ilipitisha majina ya makada watakaopeperusha bendera ya chama hicho kuwania ubunge, huku ikikata majina ya vigogo kadhaa wakiwamo walioongoza kura za maoni majimboni.

Profesa Mpangala alisema CCM imefanya juhudi kubwa katika kuchambua majina ya wagombea wa nafasi hizo, lakini kwa kukata majina ya waliongoza, anaona kuna ukakasi ambao unamfanya asiunge mkono uamuzi huo.

Alisema wengi wa wagombea waliopita kwenye kura za maoni, walipitishwa na NEC kuwania nafasi hizo, lakini kuna wachache ambao hawakushinda katika kura za maoni, kupitishwa kwao ni kinyume cha matakwa ya kidemokrasia.

"Kuna walioshika nafasi ya 2,3 na 4 lakini majina yao yamepitishwa na NEC kuwania ubunge. Sina raha nayo kwa sababu yameenda kinyume cha matakwa ya maoni ya wananchi ambao ni wajumbe," alisema Profesa Mpangala.

Aliongeza kuwa kama waliangalia vigezo kama vile rushwa na kosoro nyingine zilizotokea kwa mujibu wa kanuni za chama hicho, haziwezi kuwa sababu za msingi kwa kuwa wagombea wote walitaka kushinda, hivyo ilikuwa rahisi kuchafuana.

"Tuhuma za rushwa siyo kitu ambacho kina uhakika sana kwa sababu kama waliokuwa wanaogombea ni wengi, ni wazi kuwa kulikuwa na kuchafuana kwa kashfa ili walioshindwa wapitishwe na chama hicho," alisema Profesa Mpangala.

Akizungumzia uwiano wa wanawake na wanaume katika uteuzi huo, msomi huyo alisema idadi ya wanawake waliojitokeza ilikuwa ndogo kulinganisha na wanaume na ndiyo sababu hata idadi ya walioteuliwa imekuwa ndogo pia.

"Suala la kufikia usawa wa kijinsia bungeni kuwa 50 kwa 50 bado ni tatizo kwa sababu idadi ya wanawake wanaojitokeza kuwania ubunge wa majimbo ni ndogo, wengi wanajikita katika ubunge wa viti maalum," alifafanua.


**MARCAS**
DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD.

**MNADA WA HADHARA**

**MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONERS LTD,** kwa idhini tuliyopewa na Hughes Agricuture (T) Ltd, P.O. Box 75344 Dar es Salaam tutauza matrekta (10) kwa njia ya mnada; mnada huo utafanyika katika ofisi za Hughes Agriculture, maeneo ya Tazara karibu na Daraja Mfugale, siku ya **5th Septemba, 2020.**

Wanunuzi wote mnakaribishwa kukagua matrekta tarehe **4th Septemba, 2020** kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9 alasiri.

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mshindi atalipa 25% papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka na kiasi kinachobakia yaani asilimia 75% italipwa ndani ya siku (14) baada ya siku ya mnada, mnunuzi atakaeshindwa kulipa asilimia 75% zilizobakia atapoteza ushindi wake na hatarudishiwa kiasi cha awali cha 25% na mali hii itanadishwa tena.
2. Bidhaa zitauzwa kama zilivyo.
3. Wanunuzi watatakiwa kufika na vitambulisho vyenye picha zao ambavyo vinatambulika na serikali.
4. Mnunuzi atalipa gharama za kodi na uhamisho.
5. Sio lazima mnunuzi mwenye bei ya juu kuwa mshindi, dalali ana haki ya kumchagua mnunuzi atakae kidhi vigezo

**Kwa maelezo zaidi wasiliana kwa simu; 0713268383/0752722222**

# Wasichana wafunika tena matokeo kidato cha sita

**Na Rahma Suleimman,**
ZANZIBAR




Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonde, akitoa taarifa ya matokeo ya kidato cha sita kwa waandishi wa habari mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

BARAZA la Mitihani (NECTA), limetangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha sita uliofanyika kaunzia Juni 29, mwaka huu, ufaulu ukionyesha shule za serikali zimefanya vizuri huku wasichana waking'ara katika matokeo hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar, Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Dk. Charles Msonde, alisema ufaulu kwa jumla unaonyesha kupanda kwa asilimia 0.03. Mwaka 2019 ufaulu ulikuwa asilimia 98.32 na mwaka huu ni asilimia 98.35.

Alisema ubora wa ufaulu umezidi kuimarika kwa kuwa idadi ya watahiniwa waliofaulu vizuri katika daraja ka kwanza hadi la tatu imeongezeka kwa asilimia 1.13 kutoka 96.61 mwaka 2019 hadi asilimia 97,74 mwaka huu.

Dk. Msonde alisema takwimu za matokeo zinaonyesha ubora wa ufaulu wa wasichana kwa mwaka huu ni mzuri zaidi kulinganishwa na wavulana kwa asilimia 0.89.

Alisema ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliopata watahiniwa wa shule unaonyesha kuwa jumla ya watahiniwa 72,230 (asillimia 97.74) wamefaulu katika daraja la kwanza hadi la tatu wakiwamo wasichana 31,786 (asilimia 98.24) na wavulana ni 40,444 (asilimia 97.35).

"Baraza la Mitihani Tanzania litafanya uchambuzi wa kina wa matokeo haya kwa kila somo na kutoa machapisho ya uchambuzi huo yatakayowasilishwa kwa wadau wa elimu, zikiwamo shule zote za sekondari za juu nchini kwa lengo la kuwawezesha walimu kutumia taarifa za uchambuzi katika kuboresha ufundishaji shuleni," alisema.

Dk. Msonde alisema kuwa jumla ya watahiniwa 85,499, walisajiliwa kufanya mitihani ya kidato cha sita mwaka huu wakiwamo wasichana 36,168 na wavulana 49,331, ambapo watahiniwa wa shule walikuwa 74,753 na wakujitegemea 10,746.

Alibainisha kuwa kati ya watahiniwa hao 85,499 waliosajiliwa, 84,212 walifanya mitihani na 1,287 hawakufanya mitihani kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za ugonjwa na utoro.

Alifafanua kuwa watahiniwa 82,440 wamefaulu (wasichana 35,486 na wavulana ni 46,954). Mwaka 2019 waliofaulu walikuwa 88,069.

"Watahiniwa wa shule waliofaulu mwaka huu ni 73,537 ambapo wasichana ni 32,255 na wavulana ni 41,282. Mwaka 2019 watahiniwa 78,666 walifaulu mitihani yao," alisema.

Alisema watahiniwa wa kujitegemea waliofaulu mwaka huu ni 8,903 kulinganishwa na 9,403 wa mwaka jana.

Kiongozi huyo wa baraza alisema watahiniwa watano wamefutiwa matokeo yao kwa sababu ya udanganyifu.

**SHULE 10 BORA**

Alizitaja shule 10 zilizofanya vizuri zaidi katika mtihani huo kuwa ni Kisimiri ya Arusha (serikali), Kemebos Kagera (binafsi), Ahmes Pwani (binafsi), Mzumbe Morogoro, Tabora Girls, Tabora Boys, Ilboru ya Arusha, Kibaha, Mwandet ya Arusha na Dereda ya Manyara, zote za serikali.

**SHULE 10 BORA MIAKA 3 MFULULIZO**

Dk. Msonde alizitaja shule 10 zilizoongoza kwa ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo kuwa ni Golden Ridge ya Geita (binafsi), Igunga ya Tabora, Machame Girls ya Kilimanjaro, Liwale Day ya Lindi, Nyanduga ya Mara (serikali), Edmund Rice Sinon ya Arusha (binafsi), Mkugwa ya Kigoma (serikali), Ruhuwiko ya Ruvuma (binafsi) na Kilosa ya Morogoro (serikali).

**SHULE 10 ZILIZOSHUKA**

Alizitaja shule 10 zilizoshuka kiufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Dk. Olsen ya Manyara (serikali), Marian Boys ya Pwani (binafsi), Mpendae ya Mjini Magharibi (serikali), Airport na Swilla za Mbeya (binafsi), Magufuli ya Geita (serikali), Mudio Islamic Seminary ya Kilimanjaro (binafsi), Kibakwe ya Dodoma, Lupa ya Mbeya na Kiembe Samaki A Islamic ya Mjini Magharibi (zote za serikali). Baraza hilo pia lilitangaza mikoa mitatu iliyofanya vizuri zaidi kwa mwaka huu kuwa ni Lindi, Mtwara na Simiyu na mikoa mitatu ambayo imeongeza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo ni Lindi, Simiyu na Ruvuma.

**WAKALI WA SAYANSI**

Aliwataja watahiniwa waliong'ara upande wa masomo ya sayansi kuwa ni Alex Mbogo - Kibaha, Longnus Mgaza - Ilboru, Claud Kitumbika - Tabora Boys (PCB), Mwesiga Rwegerera - Kismiri, Maria Gambaloya - Mariana Girls, Marietha Mondea - St. Mary's Mazinde Juu, Abuu Mtambo - Kisimiri, Asterius Mayaya - Mzumbe, Edward Ndonyo - Ilboru na Nisha Nkya - Feza Girls (PCM).

**WASICHANA 10 BORA**

Maria Hewa (Mariana Girls), Marietha Mondea (St. Mary's Mazinde Juu), Nisha Nkya (Feza Girls), Clara Malando (Tabora Girls), Elizabeth Mangu (Marian Girls), Rosemary Kilembe (Feza Girls), Anna Peter (Pandahill), Elizabeth Kway (St. Mary's), Elizabeth Ngwalu (St. Marry's Mazinde Juu) na Carolina Kabebeka (Ngaza).

**WAVULANA 10 BORA**

Alex Mbogo (Kibaha), Longnus Mgaza (Ilboru), Claud Kitumbika (Tabora Boys), Mwesiga Rwegerera (Kisimiri), Abuu Mtambo (Kismiri), Asterius Mayaya (Mzumbe), Edward Ndonyo (Ilboru), Ahazi Jaredi (Tabora Boys), Emerson Faustine (Mahuwi) na Samwel Malembo (Mzumbe).

**10 BORA LUGHA NA SANAA**

Joseph Masangula (Kisimiri), Ndhuhirubusa Januari (Milambo), Theontius Theobald (Kisimiri), Priscus Thomas (Lyamungo), Mariam Kimario (St. Mary's Mazinde Juu), Erasto Magavilo (Ahmes), Stephen Mlogolo (Ndanda), Dina Rugaimukamu (St. Mary, Kilimanjaro) na Cuthbert Ramat (Ahmes).

**WASICHANA BORA LUGHA NA SANAA**

Mariam Kimario (St. Mary's Mazinde Juu), Ilonga Sigonda (St. Mary's Mazinde Juu), Dina Rugaimukamu (St. Mary, Kilamnjaro), Gloria Vasonga (St. Mary Mzinde Juu), Mary Chami (Tabora Girls), Catherine Willium (Feza Girls), Rebeka Mwaibingila (Patrick Mission), Elizabeth Kimario (St. Mary's Mazinde Juu), Esther Maboja (Ahmes) na Zainabu Mahungo (Kisimiri).

**WAVULANA BORA LUGHA NA SANAA**

Joseph Masangula (Kisimiri), Ndhuhirubusa Jamali (Milambo), Theontius Theobald (Kisimiri), Priscus Thomas (Lyamungo), Erasto Magavilo (Ahmes), Stephen Mlogolo (Ndanda), Cuthbert Ramat (Ahmes), Mjahidina Ali (Kisonsera), Ashfaq Ahmed (Kemebos) na Harold Sanja (Berege).

**WAKALI WA BIASHARA**

Samiya Ali (St. Christina Girls), Augenia Mashaula (Weruweru), Marina Somoka (Patrick Mission), Sheila Ntisi (Baobap), Tatu Kikanda (Benjamine William Mkapa), Saadia Yussuf (Shaban Robert), Kalumuna John (Kemebos), Consolatha Mgina (Miringa), Apaikunda Olotu (Wereweru) na Abdulrahman Mkanjima (Zanzibar Commercial).

**WASICHANA BORA BIASHARA**

Samiya Ali (St. Christina Girls), Augenia Mashaula (Weruweru), Marina Somoka (Patrick Mission), Sheila Ntisi (Baobab), Tatu Kikanda (Benjamine William Mkapa), Saadia Yussuf (Shaban Robert), Consolatha Mgina (Miringa), Apaikunda Olotu (Wereweru), Zubeida Hemed (Chasasa) na Rayer Nassoro (Weruweru).

**WAVULANA BORA BIASHARA**

Kalumuna John (Kemebos), Abdulrahman Mkanjima (Zanzibar Commercial), Albert Sunghwa (St. Joseph's Cathedral), Ladislaus Budili (Tusiime), Rajabu Mcomvu (Kibaha), Mussa Wilson (Bondeni), Allen Jonathan (Kibaha), Godfrey Assenga (Eagles), Grayson Kimaro na Samwel Ngowi (wote St. Mary, Kilimanjaro).




Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo akipokea kitambulisho kutoka kwa Brigedia Jenerali mstaafu, Mary Hiki, baada ya kuwaaga Maofisa Wakuu 16 wa Jeshi hilo, waliostaafu utumishi wa umma katika hafla iliyofanyika viwanja vya Kambi ya Twalipo, eneo la Mgulani, jijini Dar es Salaam jana.**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbunge atoa neno matukio ya moto ofisi za CHADEMA

**Na Thobias Mwanakatwe**

MFULULIZO wa matukio ya kuungua moto kwa ofisi za Chama cha Demokrasia na Manedeleo (CHADEMA) umemshtua Mbunge wa zamani wa Kigamboni, Frank Magoba.

Kutokana na matukio hayo, Magoba amevishauri vyombo vya ulinzi na usalama kuwasaka wahusika na hatimaye kuchukuliwa hatua za kisheria

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Magoba alisema vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kuchukua hatua haraka kukomesha matukio hayo ambayo kama yataendelea kujitokeza katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu, yataleta mtazamo tofauti ndani na nje ya nchi. "Rais (John Magufuli) alishasema kampeni za uchaguzi mwaka huu zitakuwa za kistaarabu. Sasa matukio haya yaliyoanza kujitokeza hayafai na yanapaswa kukemewa na kulaaniwa kwa nguvu zote na wapenda amani nchini," alisema.

Magoba alisema Tanzania inasifika duniani kwa kuwa na amani, hivyo uchaguzi mkuu wa mwaka huu hakuna sababu kwa Watanzania kuivuruga kutokana na tofauti zao za kiitikadi.

Alisema wananchi watoe ushirikiano kwa vyombo vya dola ili wahusika wapatikane na kuchukuliwa na hatua kwa mujibu wa sheria.

Kuhusu wagombea waliokatwa katika Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema wanapaswa kukubali uamuzi wa vikao vya juu vya chama, hivyo waunganishe nguvu kuhakikisha chama chao kinapata ushindi.

"CCM ina utaratibu mzuri wa kupata wagombea waliokatwa wakubali yaishe wasianze kuweka bifu, lazima watambue kuwa katika uchaguzi kuna kushinda na kushindwa," alisema.

"Navipongeza sana vyama vyote vya siasa kwa kuonyesha ukomavu wa hali ya juu katika mchakato mzima wa kupata viongozi watakaowakilisha wananchi katika majimbo na katika kata mbalimbali hapa nchini," alisema.

Agosti 13, mwaka huu, watu wasiojulikana walidaiwa kuvamia na kuchoma moto jengo la ofisi ya CHADEMA Kanda ya Kaskazini zilizoko Arusha na kusababisha uharibifu wa mali ambazo thamani yake haijajulikana.

Pia Agosti 19, ofisi ya CHADEMA, Wilaya ya Mbeya Mjini ziliungua moto huku watu wasiojulikana wakidaiwa kuhusika na kadhia hiyo iliyosababisha kuteketea baadhi ya nyaraka muhimu zikiwamo fomu za wagombea ubunge wa viti maalumu.

# Mtoto wa mwaka mmoja afa ajali ya basi

**Na Restuta Damian,** MULEBA

WATU wanane akiwamo mtoto wa umri wa mwaka mmoja, wamefariki dunia kutokana na ajali ya basi.

Mbali na vifo hivyo, watu wengine 27 wamejeruhiwa katika ajali hiyo iliyohusisha basi la kampuni ya Sabuni Express lenye namba za usajiliT.392 AZB katika eneo la Kyamalebe kijiji cha Rutenge, Muleba mkoani Kagera

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana na kusema idadi kamili ya abiria waliokuwamo haijafahamika.

Malimi alisema miili ya marehemu imepelekwa kuhifadhiwa katika Hospital Teule ya Wilaya, Rubya na majeruhi kupelekwa kwa matibabu katika Hospitali ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ya Ndolage inayomilikiwa na kanisa hilo Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.

Alisema katika majeruhi hao 27, Kuna majeruhi wanne walio mahututi zaidi ambao walipelekwa mapema hospitalini kwa matibabu.

Kamanda Malimi aliwataja marehemu waliotambuliwa ni Ruhoya (49) mkazi wa Nshamba, Philibert Katabazi (62) mkazi was Nshamba, Pascazia Pastory (88) mkazi kishanda, Vestina Cornel (39) mkazi wa Buganguzi, Golet Adolf (42) mkazi wa Nshamba na mtoto Prisca Revocatus mkazi wa Nshamba

Alisema chanzo cha ajari hiyo ni mwendo kasi, hivyo dereva kushindwa kudhibiti gari katika mteremko mkali kwenye enen la ajali.

"Hapa ilipotokea kuna jiwe kubwa inaonekana lilimshinda dereva kukunja kona na safari (ruti) za gari hilo siyo halisii," alisema Malimi,

Baada ya ajali hiyo, kwa mujibu wa Kamanda malimi, dereva wa gari hilo alikimbia kusikojulikana na polisi wanaendelea kumsaka ili kumchukulia hatua za kisheria.

# Kijazi Mkuu mpya UDOM

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Balozi John Kijazi kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema uteuzi huo ulianza rasmi Agosti 21, mwaka huu.

Balozi Kijazi ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, anachukua nafasi ya Rais mstaafu Benjamin Mkapa, ambaye alifariki dunia hivi karibuni.

# Wateja wakata tiketi mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Zantel wataanza kununua tiketi za usafiri wa boti za ZanFast Ferries kwa urahisi kwa kulipa kupitia mtandao wa fedha wa Ezypesa.

Hatua hiyo inatokana na kampuni hiyo kuingia ubia na kampuni ya usafirishaji ya Vigor Group ambayo inamiliki boti za ZanFast Ferries ili kuboresha huduma za ukataji tiketi. Kampuni hiyo ni moja ya watoa huduma za usafiri wa majini kati ya Zanzibar na Dar es Salaam.

Akizungumzia hatua hiyo, Mkuu wa Zantel-Zanzibar, Mohammed Mussa, alisema hatua hiyo imelenga kurahisisha upatikanaji wa huduma za ukataji tiketi kwa abiria hivyo kuboresha maisha ya wateja wao.

"Kwa kupitia Ezypesa tunahakikisha wateja wanafanya malipo yao kwa urahisi zaidi, mahali popote na wakati wowote.Ushirikiano wetu na ZanFast Ferries unawapa wateja uhuru zaidi wa kununua tiketi na kupunguza muda na mchakato wa kununua tiketi," alisema Mussa.

Ili kupata tiketi, mteja atatakiwa kupakua application ya ZanFast Ferries kisha kwenda Kata tiketi, chagua Ezypesa na fanya malipo. Baada ya kukamilisha malipo mteja atapokea ujumbe mfupi (SMS) Pamoja na tiketi laini (e-ticket) itakayotumika siku ya safari.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Vigor Group, Abdallah Turky, alisema kampuni hiyo imejidhatiti katika kuboresha huduma za usafiri kwa kuhakikisha inawapa wateja njia rahisi na za kidigitali za kufanya malipo ya tiketi.

"Ushirikiano baina yetu na Ezypesa umetanua wigo wa njia za malipo sanjari na App yetu ya ZanFast Ferries ambazo zinampa mteja uhuru wa kununua tiketi mahali popote alipo," alisema.

Aliongeza kuwa kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na Zantel katika kuleta huduma na bidhaa za kidigitali ili kurahisisha malipo kwa wateja wake.

Wateja watakaofanya malipo kwa Ezypesa watatumia tiketi laini (e-ticket) badala ya tiketi za kawaida na watatakiwa kuwa nayo siku ya safari.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Mafuriko Simba Day lipo la kujifunza mashabiki, klabu*

**LEO** mabingwa wa soka nchini, Klabu ya Simba, wanahitimisha kilele chao cha Wiki ya Simba, kwa tamasha maalum maarufu kama Simba Day, linalofanyika katika Uwanja wa Mkapa pamoja na ule wa Uhuru kwa wakati mmoja.

Kwa wiki nzima hadi kufikia kilele hicho leo, wanachama, mashabiki, wachezaji pamoja na viongozi wa klabu hiyo wamekuwa wakijihusisha katika shughuli mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na kusaidia watu wenye mahitaji maalum.

Katika tamasha hilo ambalo, Simba italitumia kutambulisha jezi, wachezaji wake wa msimu mpya wa 2020/21 na kuuza vifaa vyao mbalimbali vya michezo, mwaka huu, baada ya shughuli zote itahitimisha kwa kucheza mechi ya kirafiki jioni dhidi ya Vital'O ya Burundi.

Hata hivyo, uongozi wa Simba umeeleza kwamba umelazimika kuomba kibali cha kutumia viwanja viwili ili kuwezesha mashabiki wao wote kushuhudia tamasha hilo, ambapo watakaotumia Uwanja wa Uhuru watashuhudia kupitia runinga huku kingilio kikiwa bei poa ya Sh. 2,000 tu. Kwa Uwanja wa Mkapa ambapo shughuli zote zitashuhudiwa mubashara, Simba imetangaza kuwa kiingilio ni kati ya Sh. 7,000, Sh. 20,000, Sh. 30,000, Sh. 40,000 na cha juu kabisa kikiwa ni Sh. 150,000.

Licha ya viingilia hivyo kuonekana kuwa vya juu, tangu juzi upatikanaji wa tiketi umekuwa changamoto kubwa huku ukitawaliwa na foleni ndefu, jambo ambalo linaonyesha leo katika viwanja hivyo itakuwa ni zaidi ya mafuriko katika, huku Simba ikijitengenezea kiasi kikubwa cha fedha.

Hakika hiki ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Simba na hata serikali kwa ujumla, jambo ambalo litasaidia klabu hiyo kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za uendeshaji kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano mingine ikiwamo ya kimataifa.

Kwa ujumla tumevutiwa sana na uhamasishaji uliofanywa na viongozi wa Simba pamoja na mbinu walizotumia kwa kumualika msanii wa muziki, Diamond Platinumz kwani wapo ambao watahudhuria tamasha hilo, kwa ajili tu ya kumuona mwanamuziki huyo pamoja na wengine wakati wakitumbuiza uwanjani hapo.

Kwa hilo, tunaona kuna kitu cha kujifunza kwa klabu nyingine ambazo nyingi husubiri kujiendesha kwa kutegemea mapato ya mlangoni pekee pindi msimu unapofunguliwa, jambo ambalo husababisha kujiendesha kwa tabu huku zikishindwa kuwalipa wachezaji kwa wakati.

Lakini pia, kwa tamasha hilo, hata Simba yenyewe ina jambo la kujifunza katika kuhamasisha mashabiki wake kuhudhuria mechi za Ligi Kuu pindi msimu unapoanza hasa ukizingatia mechi kuonyesha mubashara kupitia Azam TV imekuwa moja ya sababu ya mahudhurio viwanjani kupungua.


Kadhalika, kwa tamasha kama hili lililofanyika Dar es Salaam, Klabu ya Simba ingeweza kutengeneza fedha za kujiendesha karibu msimu mzima, kama baada ya hapo lingehamia, Mbeya, Mwanza, Arusha, Dodoma, Kigoma, Kagera, Iringa, Tanga, Zanzibar na mikoa mingine, kwani klabu hiyo na hata Yanga zina mashabiki wengi karibu mikoa yote nchini.

Tunachokiona katika tamasha hilo la leo, kuna haja ya kila mechi timu mwenyeji kutafuta wasanii maarufu kuanza kutumbuiza uwanjani kabla ya mechi kuanza, jambo ambalo litachangia kwa kiasi kikubwa mahudhurio ya mashabiki kuongezeka, kwani wapo watakaofuata burudani ya muziki, soka na wengine vyote kwa pamoja.

Lakini pia tunatamani kuona mashabiki wakiendelea kujitokeza kwa wingi viwanjani kuzisapoti timu zao, kama ambavyo imetokea Simba Day leo, kwa kwa tiketi za tamasha hilo kutafutwa kwa almasi.

Tunatamani kuona soka letu linafikia hatua mashabiki wananunua tiketi za msimu kama ilivyo Ulaya, jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa klabu kukuza uchumi wao na kuwafanya wadhamini zaidi kujitokeza kuzidhamini hivyo ligi kuzidi kuwa ya ushindani mkubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Damu ni damu si kitarasa*

**'KITARASA'** ni aina ya ndizi inayotoa utomvu mwekundu. Maana ya kichwa cha makala haya ni kwamba damu haiwezi kufanana na kitarasa. Methali hii inatufunza kwamba uhusiano wa kidamu ni muhimu sana. Pia husemwa damu ni nzito kuliko maji.

'Uzalendo' ni hali ya mtu kuwa na nasaba ya asili ya nchi. Hali ya mtu kujitolea kwa hali na mali kwa ajili ya nchi yake. Watanzania twapaswa kupendana kwa dhati badala ya kuchukiana na kuhasimiana. Yashangaza kuwa Yanga au Simba inapocheza na timu ngeni kutoka nje ya nchi, wageni hao hushangiliwa mno na wapenzi wa Yanga au Simba. Kisa ni chuki kati yao!

Kwa hiyo mojawapo ikifungwa huwa chereko kwa upande mwingine na kuizomea mno timu ya nyumbani iliyoshindwa! Huo ni uzuzu, yaani uwezo mdogo wa mtu kufahamu mambo; hali ya mtu kutolijua jambo linaloendelea. Pia ni uzulufu, yaani tabia ya mtu kufanya jambo lisilolingana na umri wake au maadili ya jamii yake. Uzuzu na uzulufu hufanywa na watu wazima wenye akili timamu! Wahenga walisema "Ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni." Maana yake ukishangaa kutokana na miujiza ya Musa utashtuliwa na matendo ya Firauni. Ndivyo walivyo mashabiki mbumbumbu wa Yanga na Simba wanavyochekana mitaani, mojawapo inaposhindwa na timu za nje ya nchi! Eti husema bila soni kuwa bora imekuwa hivyo, kwani Yanga au Simba ingeshinda, watu wasingelala kwa shangwe. Kuna ubaya gani watu kufurahia timu ya nyumbani inapoishinda timu ya ugenini?

Nadhani hata wageni wanaoshangiliwa sana kila wanaposhindana na timu zetu hutulinganisha na majuha. Ndo maana huja na jezi zao kuwauzia watu wasiokuwa waungwana, nao huzinunua na kuzivaa siku ya kupambana na Yanga au Simba! Jamani tuchekane wakati timu zetu zinapofungana lakini si kushangilia zinapofungwa na timu ngeni.

Huu ni ubwege uliopituka kwa mashabiki wa Yanga na Simba. Ndo maana sikubaliani na wanaoziita timu hizo 'watani wa jadi' kwani watani hawaombeani mabaya bali husaidiana katika shida. Kwa hiyo kama wangefuata maana ya utani, yaani taratibu au desturi za kimila zinazowafanya watu wanaojuana kuambiana au kutendeana jambo lolote la mzaha bila kuleta chuki au kero, wasingeshangilia wakati mojawapo ikipoteza mchezo kwa timu inayotoka nje ya nchi. Kwa hali hiyo udugu wa Yanga na Simba u'wapi?

Simba ambao wametwaa Kombe la Ligi Kuu mara tatu mfululizo msimu uliopita, itaiwakilisha Tanzania kwenye mechi za kimataifa Kanda ya Afrika. Kwa maana hiyo Watanzania wote bila kujali tofauti zetu, makabila yetu, mikoa na timu tuzipendazo, twapaswa kuiombea Simba na kuishangilia kwa bidii na upendo wa nchi yetu ili ipate ushindi katika mechi za kimataifa na ikibidi, hata kutwaa Kombe la Afrika, inshallah (apendapo Mwenyezi Mungu).

Itakaposhinda, haitakuwa ushindi wa Simba tu bali ushindi wa Watanzania wote na kuifanya nchi yetu itambuliwe na kuheshimiwa kwenye mchezo wa kabumbu. Timu yoyote itakayocheza mechi za kimataifa, twapaswa kuweka kando tofauti na chuki zetu kwa kuishangilia kwa bidii na dhati, yaani umakini wa moyo, na nia thabiti ya kufanya kitu kwa uaminifu.

Aidha, kuna timu ya Namungo iliyoingia Ligi Kuu iliyomalizika hivi karibuni na kugombea Kombe la Azam. Ingawa ilifungwa na Simba kwa mabao 2-1, imepata nafasi ya kucheza mechi za kimataifa. Hawa nao wanastahiki kabisa kuungwa mkono na kushangiliwa kwa kila hali ili kuwapa ari ya kucheza kwa bidii na ikiwezekana watwae Kombe linaloshindaniwa. Sifa itakuwa kwa Tanzania.

"Ujirani mwema hutengeneza njia." Hii ni methali ya kutumiwa kutukumbusha kuwa uhusiano au uelewano mzuri kati ya watu ni kitu muhimu maishani. Twahimizwa kudumisha uhusiano mzuri na majirani zetu.

Kadhalika, kuna uwezekano wa Yanga nayo kuingizwa kwenye mechi za kimataifa kwa kushika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ya msimu uliopita. Hawa nao kama itakavyokuwa kwa Simba na Namungo, wanastahiki kushangiliwa kwani zote ni timu za Tanzania.

Yanga na Simba zina rekodi zao katika mechi za nyumbani. Yanga imetwaa Kombe la Ligi Kuu mara nyingi zaidi ya timu zote ikiwamo Simba. Ilichofanya Yanga kwa mechi za kimataifa ni kufika nusu fainali ya Kombe la Afrika na mara nyingi ikidharauliwa na kuonewa na timu za Waarabu.

Simba nayo imeweka rekodi ya kutwaa makombe matatu na ngao humu nchini msimu uliopita, jambo ambalo halikuwahi kufanywa na Yanga kwa msimu mmoja. Katika mechi za kimataifa, Simba ilifika fainali ya Kombe la Afrika ilipofungwa mabao 2-0 mbele ya Rais Ali Hassan Mwinyi jijini Dar es Salaam.

HABARI PICHANI

# UCHUKUAJI WA FOMU ZA UTEUZI KWA WAGOMBEA UBUNGE



Mgombea wa ubunge Jimbo la Mbogwe kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Nicodemus Maganga, akizungumza na wananchi na wanachama wa chama hicho, Wilaya ya Mbongwe, mkoani Geita jana, baada ya kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi hiyo kwa Msimamizi wa Uchaguzi, Elias Kayandabila. **PICHA: SHABAN NJIA**



Mgombea ubunge wa Jimbo la Manonga, mkoani Tabora (CCM), Seif Gulamali (kulia), akikabidhiwa fomu ya uteuzi wa kugombea kiti hicho na Msimamizi wa jimbo hilo, Wakili Revocatus Kuuli, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mgombea ubunge Jimbo la Ilala, kwa tiketi ya CCM, Mussa Zungu (kulia), akipokea fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi hiyo kutoka kwa Mkurugenzi wa ManIspaa ya Ilala ambaye pia ni Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Jumanne Shauri, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mgombea Ubunge wa Jimbo la Hai mkoani Kilimanjaro (CCM), Saashisha Mafuwe, akionyesha fomu ya uteuzi wa kugombea kiti hicho jana, baada ya kukabidhiwa fomu hiyo na Msimamizi wa Ubunge wa jimbo hilo, Yohana Sintoo (hayupo pichani). **PICHA: GODFREY MUSHI**




Aliyewahi kuwa mbunge wa jimbo la Dodoma mjini kupitia CCM mwaka 2010 mpaka 2015, Dk. David Malole (kushoto), akikabidhiwa fomu ya uteuzi wa kugombea ubunge wa jimbo la Dodoma Mjini, kupitia chama cha ACT Wazalendo na Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Msekeni Mkufya, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Solwa, mkoani Shinyanga, Hoja Mahiba, (kushoto), akimkabidhi fomu ya uteuzi kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Ahmed Salum, jana , kwa ajili ya kugombea ubunge wa Jimbo hilo, kupitia tiketi ya CCM. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wajasiriamali waelimishwa usahihi vipimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo nchini (WMA), imeanza kampeni ya kuwaelimisha wajasiriamali wadogo kuhusu umuhimu wa kuwa na vipimo sahihi kwenye biashara zao.

Mafunzo hayo ambayo yatakuwa endelevu ili kuwafikia wajasiriamali wengi wadogo nchini, yalifanyika jana kwenye ofisi za WMA jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia umuhimu wa vipimo sahihi kwenye mafunzo hayo, Kaimu Meneja Upimaji, Pastory Almachus, alisema vipimo sahihi hutumiwa na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kupata takwimu sahihi.

Meneja huyo alitoa mfano kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hutumia kigezo cha vipimo katika ukusanyaji mbalimbali wakati inapotoza kodi kwa bidhaa mbalimbali.

Alisema kwenye miundombinu na usafirishaji, vyombo vya usafiri hubeba bidhaa, mizigo na abiria kulingana na uwezo, hivyo kuepusha ajali na uharibifu wa miundombinu kama barabara na reli na kupunguza matukio ya ajali.

Hata wakulima alisema hutumia vipimo sahihi katika matumizi ya pembejeo wakati wa uzalishaji na wakati wa kuuza mazao ili kupata thamani kulingana na gharama alizotumia.

Aidha, taarifa zinazotolewa na sekta mbalimbali kuhusu uzalishaji, biashara na uchumi hutegemea vipimo nazo husaidia kujua mchango wa kila sekta katika pato la taifa kwa usahihi.

Alisema bidhaa zinazotengenezwa viwandani hutegemea vipimo ambavyo hutumika kupimia malighafi na mahitaji mengine na kwamba bidhaa zikishatengenezwa bado hutegemea usahihi wa vipimo wakati wa kufungashwa katika ujazo, urefu au uzito tayari kwa kusambazwa katika masoko.

Kwa mujibu wa Almachus, miongoni mwa majukumu ya wakala ni kuhakikisha vipimo vyote vinatumika kwenye biashara na huduma mbalimbali kama vile afya, usalama na mazingira.

Majukumu mengine ya wakala, alisema ni kukagua bidhaa zilizofungashwa ku toka nje ya nchi na zile zinazozalishwa hapa nchini na kusimamia matumizi sahihi ya vipimo kwa njia ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara.

# Ndikilo awashia moto viongozi mizigo

**Na Julieth Mkireri,**
KISARAWE

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amewataka viongozi katika ngazi mbalimbali kuacha tabia ya kusubiri viongozi wa kitaifa kutatua kero za wananchi badala yake kila mmoja awajibike katika nafasi yake.

Pia amewataka watumishi wa umma na sekta binafsi mkoani hapa kila mmoja kutimiza wajibu wake katika kuwatumikia wananchi ikiwa ni pamoja na kutatua kero zinazowakabili kwa wakati.

Ndikilo alitoa agizo hilo juzi mjini hapa, akiwa katika mkutano na wananchi wakati wa ziara yake ya kikazi kusikiliza kero za wananchi anayoifanya katika mkoa akiambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa pamoja na watendaji.

"Tusisubiri viongozi wa ngazi ya kitaifa wafike kutatua kero za wananchi kwenye vitongoji na kata, hii si sawa. Jipangeni kuwasikiliza wananchi na kutafuta ufumbuzi wa vikwazo vya maendeleo kwao na pia mnapotatua kero, jaribuni kutumia mbinu tofauti," alisema.

Mhandisi Ndikilo alisema kila mmoja anatakiwa kusimama katika nafasi yake kuhakikisha hakuna kero ambayo iko ndani ya uwezo wake na haijapatiwa ufumbuzi kwa wakati.

"Wananchi leteni taarifa kama kuna mtumishi wa mkoa ambaye hawajibiki ipasavyo kwenye eneo lake. Huu sio wakati wa kuendelea kuwavumilia watu ambao hawawajibiki katika nafasi zao," alisisitiza Ndikilo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani, Dk. Delphine Magare, alisema hatakuwa tayari kumvumilia mtendaji ambaye hatatekeleza ipasavyo majukumu yake na kwamba yeyote atakayekwenda kinyume atafikisha taarifa kwa mkuu wa mkoa.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, aliwataka watendaji kufanya kazi na kumsaidia Rais John Magufuli badala ya kuwa mzigo na kushindwa kutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

" Wataalamu wafanye kazi zao, mambo mengi wanaweza kuyamaliza kabla hayajafika mbali, wazitendee haki dhamana zao, wasilundike kero za wananchi na kugeuka kuwa mizigo kwa kushindwa kusimamia majukumu yao," alisema.

Katika mkutano huo wananchi wengi walilalamikia suala la fidia ambalo alielekeza idara husika kulitafutia ufumbuzi wa haraka.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki (kushoto), akiwa na mwenyeji wake Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano Vodacom Tanzania, Rosalynn Mworia (wa pili kushoto), na maofisa aliofuatana nao wakibadilishana mawazo, alipofanya ziara ya kikazi katika kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), Dk. Maduhu Isaack Kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mitaji midogo yakwamisha urasimishaji

**Na James Kandoya**

UWEZO mdogo kifedha wa kampuni binafsi za upangaji na upimaji ardhi nchini kumudu gharama, umetajwa kuwa moja ya changamoto inayodhorotesha kasi katika kufanikisha azma hiyo.

Hayo yalibainika jana jijini Dar es Salaam kwenye kikao kati ya wataalam wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na halmashauri zake walipokutana na Kamati za Urasimishaji na Wawakilishi wa kampuni hizo kujadili changamoto na ufumbuzi wake.

Kiongozi wa Kikosi Kazi kutoka wizarani, David Malisa, alisema wizara iliamua kuunda tume baada kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ili kufanya tathmini na ufuatiliaji wa kazi zilizofanywa na kampuni hizo.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, asilimia kubwa ya kampuni za upimaji na urasimishaji, zimemaliza muda wa mikataba yao kabla ya kazi kukamilika.

"Tuko hapa kwa maelekezo ya wizara yenye dhamana ya ardhi kuhakikisha tunapata ufumbuzi wa sababu zilizofanya kukwama kwa urasimishaji," alisema.

Mwakilishi wa Kampuni ya Mataro Developers, Joel Mataro, alisema wananchi wengi wamekuwa na mwamko wa kushiriki katika urasimishaji lakini utata unajitokeza pale wanapotakiwa kulipa Sh. 150,000, kiasi ambacho kimepangwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Baada ya kutolewa hoja mbalimbali, kikosi kazi kimezitaka kampuni hizo kuhakikisha kazi inafanyika kwa watu wale ambao tayari wamelipa bila kusubiri michango ya watu wote ikamilike.

Pia kikosi kazi kimezitaka kampuni kufanya kazi bila kutegemea michango ya wananchi kama mtaji wa kufanya kazi na zimalizike kwa muda uliokubalika kwenye mkataba.

Kikosi kazi hicho kimebaini pia changamoto nyingine kuwa upitishwaji wa michoro ya mipango miji katika halmashauri ambapo kumekuwa na milolongo mirefu, hivyo kusababisha uchelewashi usio wa lazima.

"Tumeazimia kuwa kamishna wa ardhi mkoa amwandikie barua mkurugenzi ili kuzipa kipaumbele kazi za urasimishaji kuondoa ucheleweshaji usio wa lazima," alisema Malisa.






Mkurungenzi wa Elimu ya Msingi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Suzana Nyarubamba (kulia), akipokea masaada wa madawati 15 na viti vyake vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni moja, kutoka kwa viongozi wa wanafunzi wa shahada ya uzamili wa chuo kikuu cha Dodoma (UDOM), Happy Anthony (kushoto) na Elimmiliki Azaliwa, jijini Dodoma jana, uliotolewa na wanafunzi hao, kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Sechelela iliyopo katika Jiji hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wazazi wadaiwa kuwalazimisha watoto kutumia mpango wa uzazi

**Na Peter Mkwavila**, CHAMWINO

KATIKA kukabiliana na tatizo la mimba za utotoni katika Wilaya ya Chamwino, baadhi ya wazazi wenye wanafunzi wa kike wanaosoma shule za msingi na sekondari, wameanza kuwalazimisha watoto wao kutumia njia za uzazi wa mpango ili kuwakinga dhidi ya ujauzito.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mpwayungu, Ambaliche Boniface, aliyasema hayo jana katika kikao kazi cha kupanga mikakati kwenye mradi wa kutokomeza ukatili kwa kupunguza mimba na ndoa za utotoni.

Kikao hicho kilikuwa kikijadili mkakati wa mradi huo unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Women Wake Up (WOWAP) kwa ufadhili wa The Foundation For Civil Society (FCS). Akizungumza katika kikao hicho, Boniface alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakifika kituo cha afya kuomba watoto wao watumie uzazi wa mpango kama njia ya kuwakinga na ujauzito wakiwa shuleni.

"Mzazi anaona ni bora ampe mtoto wake vidonge vya kupanga uzazi au awekewe kipandikizi au kitanzi. Anaona heri mtoto apate maradhi mengine kuliko mimba," alisema.

Alisema njia hiyo si salama kwa kuwa mtoto anapowekewa njia za kumkinga dhidi ya ujauzito, atazidi kufanya ngono zaidi kwani atajihakikishia yuko huru zaidi."Wazazi hawatimizi wajibu wao. Hawakai kwenye nafasi zao, wanaona ni heri mtoto afuate uzazi wa mpango, kama ngono afanye tu ili mradi asipate mimba akafukuzwa shule," alisema.

Mganga huyo alisema watoto wanaofikishwa kituoni hapo ni wale wenye umri wa kuanzia miaka 14 na kuendelea lakini kituo hicho hakitoi huduma ya kuwafunga watoto uzazi au kutoa vidonge vya uzazi wa mpango.

Alisema sasa hivi wanashauriana na viongozi wa vijiji ili watoe elimu katika shule za msingi na sekondari ili kuondoa dhana hiyo ambayo imekuwa imeshamiri katika maeneo mengi.

"Si vizuri mtoto wa miaka 14 au 16 kuanza kutumia njia za uzazi wa mpango kwani anaweza kupata athari za kiafya hapo baadaye," alisema.

Naye Mratibu wa Dawati la Mtoto kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Sophia Swai, alisema tatizo hilo linalowakabili watumishi wa kada ya afya walioko kwenye vituo vya afya na zahanati.

"Wao wafuate maadili na miiko ya kazi zao, lakini pia wawashauri na kuwaambia madhara yake," alisema.

Alisema kutokana na zahanati na vituo vya afya vya serikali kutotoa huduma kwa wanafunzi wanaohitaji huduma, lakini wanaweza kupata huduma kwenye baadhi za zahanati na hospitali zinazokiuka maadili.

Kwa upande wake, Katekista wa Kanisa la Anglikana Kata ya Mpwayungu, Grace Omari, alisema wazazi wanaogopa mimba kuliko tatizo zima la ngono zembe ndio maana wanashauri watoto wao kutumia kipandikizi, kitanzi na vidonge vya uzazi wa mpango.

# Wachangia fedha saruji kuboresha elimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TENMET), umebaini tatizo la miundombinu ya elimu katika Wilaya ya Chemba linalochangia kuwa na kiwango cha chini kitaaluma.

Kutokana na hali hiyo, mtandao huo umetoa msaada wa mifuko 300 ya saruji na fedha taslimu Sh. milioni 11 ili kuboresha miundombinu hiyo.

Akizungumza jana wakati akikabidhi saruji na fedha hizo, Mwenyekiti wa Bodi ya TENMET ambaye pia Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kalaghe, alisema hatua hiyo imetokana na kubaini baadhi ya shule wilayani hapa kuwa na tatizo la miundombinu.

"Katika Wiki hii ya Elimu ambayo imefanyika wilayani hapa, kuna baadhi ya shule tumezitembelea na kubaini kuwapo ukosefu wa miundombinu na iliyopo kutotosheleza mahitaji, hivyo tumetoa saruji na fedha ili kusaidia ujenzi katika baadhi ya shule," alisema Dk. Kalaghe.

Alisema TENMET imeamua kufanya wiki hiyo Chemba kutokana na wilaya hiyo kuwa na mwamko mdogo kielimu.

"Tumezunguka karibia shule zote wilayani Chemba, moja ya matatizo makubwa ni miundombinu ya elimu ndiyo maana tumetoa mifuko ya saruji na fedha kwa ajili ya kuboresha," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Dk. Semistatus Shimba, aliishukuru TENMET kwa msaada huo na kuahidi utatumika kuboresha miundombinu ya elimu.

Alisema licha ya msaada huo, bado hali ya miundombinu katika halmashauri hiyo ni tatizo.

"Tunaishukuru TENMET kwa msaada huo, umefika kwa wakati lakini pia tunawashukuru kwa kufanyia Wiki ya Elimu kwani imesaidia kuibua changamoto mbalimbali," alisema.

Hata hivyo, aliwataka TENMET kujenga makao makuu yao Chemba ili kuendelea kuhimiza mwamko wa elimu.

"Nawaomba wekezeni Chemba kilomita 110 si mbali. Mkiwa hapa mtatusaidia kuboresha sekta ya elimu kwani mnakutana na matatizo ya ana kwa ana," alisema.

## Chanjo surua, Polio zawasili

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imesema chanjo ya Polio na Surua-Rubella ambazo zilipungua nchini kwa zaidi ya mwezi mmoja zimewasili huku ikiagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha zinafika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Chanjo hizo mbili zilizopungua kwa mwezi mmoja na nusu kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa cCorona.

Mkurugenzi wa Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Leonard Subi, alisema hayo jana alipotembelea ghala la kuhifadhia chanjo lililoko katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, kukagua hali ya chanjo kwa mkoa huo.


Aliwataka wazazi kuwapeleka watoto wao kupata chanjo katika vituo hivyo kwa kuwa tayari usambazaji wa chanjo hizo umeshafanyika na unaendelea kwa mikoa iliyobaki.

Dk. Subi alisema chanjo zote aina tisa ambazo zinakinga dhidi ya magonjwa 13 zipo kwenye ghala hilo na kulikuwa na upungufu wa chanjo hizo mbili ambapo kwa sasa zipo.

Alisema upungufu huo wa chanjo hizo ulitokea baada ya dunia kukumbwa na ugonjwa wa COVID-19 ambapo anga zote zilifungwa na chanjo husafirishwa kwa mnyororo baridi, kwa hiyo huhitaji usafiri wa anga.

"Tunamshukuru Rais John Magufuli kwa kulifungua anga la Tanzania ambapo, chanjo sasa zimeanza kuingia nchini na hadi sasa mikoa 13 chanjo hizi zimeshapokelewa kati ya mikoa 26, na mikoa mingine kumi na tatu ya Tanzania Bara usambazaji unaendelea kupitia Bohari ya Dawa (MSD)," alisema.

Aidha, Dk. Subi alisema usambazaji wa chanjo hizo mbili ambazo wananchi walikuwa wanazikosa, umeshaanza na watazipata kwa uhakika, huku akiagiza MSD kuhakikisha chanjo zote zimefika katika mikoa iliyosalia ya Tanzania Bara ifikapo mwishoni mwa wiki hii. "Waganga wakuu wa mikoa na halmashauri wote nchini hakikisheni chanjo hizo mnazipeleka kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya na muwajulishe wananchi kwamba chanjo zipo na zinapatikana bila malipo yeyote, wazazi na walezi pelekeni watoto wenu kupata chanjo katika mikoa yenu," alisema. Alisema serikali inaendelea kutoa fedha za chanjo, na kuweka wazi kuwa hadi sasa imetoa zaidi ya Sh. bilioni 18 kwa ajili ya ununuzi wa chanjo na kuifanya Tanzania kuendelea kuwa katika kiwango cha juu cha utoaji wa chanjo kwa zaidi ya asilimia 98 kwa miaka sita mfululizo.





# Sirro: Tumejipanga kusimamia usalama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, amesema katika kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, wamejipanga kuhakikisha amani na utulivu vinakuwapo kabla na baada ya uchaguzi.

Akizungumza jana na viongozi wa vyama vya siasa katika makao makuu ya Polisi Zanzibar, Sirro alisema madaraka hayapatikani kwa kuwaambia watu walale barabarani na kufanya fujo bali yanapatikana kwa kupiga kura kwa amani na utulivu.

IGP Sirro alisema jeshi hilo limejipanga vizuri kupambana na wale ambao watajaribu kuvunja amani na utulivu wa nchi.

Alisema si lengo la Jeshi la Polisi kutumia mabomu au risasi kwa Watanzania ambapo mabomu na siala zinanunuliwa kutokana na kodi za wananchi, hivyo silaha hizo lengo lake ni kutumika kwa ajili ya maadui. "Katika nchi za Afrika, Tanzania ni nchi ya kwanza kuwa na amani na utulivu, hivyo mataifa yote yanatuangalia katika uchaguzi na kwa bahati mbaya, maadui wetu wa mambo ya uchumi na siasa wanataka na sisi tuwe na vurugu kama walivyo wao," alisema Sirro.

Aidha, alisema vyama vyote vya siasa ni vya Watanzania na si mali ya mtu, hivyo ni aibu kuona mtu anatoka kwenda kuchoma ofisi ya chama kwa kudhani anamkomoa mtu bali husababaisha kuvunjika amani ya nchi.

Naye Kamishna wa Polisi Zanzibar, Mohamed Haji Hassan, alisema lengo la kikao hicho baina ya jeshi la polisi na viongozi wa vyama vya siasa ni kuingia katika uchaguzi bila ya vurugu.

Alisema kila mmoja anapaswa kutunza amani na utulivu nchini, wakiwamo waandishi wa habari, kwa sababu kalamu ya waandishi wa habari inaweza kuleta amani au kuvuruga amani iwapo itatumika vibaya.

Kamishna huyo alitaka kila mmoja kufuata sheria za nchi bila ya kushurutishwa ili Tanzania kuwa nchi na uchaguzi wa amani.

Kamishna Msaidizi wa Jeshi hilo, Mussa Ali Mussa, alisema uchaguzi wa Zanzibar huwa na changamoto ikilinganishwa na Tanzania Bara kwa sababu Wazanzibari huwa na utashi wa kisiasa.

Alisema viongozi wa vyama vya siasa wana wajibu wa kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na ili kufanikisha hilo ni lazima kuondokana na jazba za kisiasa.

Nao viongozi wa vyama vya siasa waliliomba Jeshi la Polisi kutenda haki kwa vyama vyote na kutoegemea upande mmoja.



Naibu Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji wa Zanzibar, Mohammed Ahmada (katikati), akishuhudia makabidhiano ya mkataba wa kuunganishwa kwenye mkongo wa taifa kati ya Pemba na Tanga ili kuboresha mawasiliano katika kisiwa cha Pemba, kulia ni Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Mussa na Mkurugenzi wa Wakala wa Miundombinu ya Mawasiliano (TEHAMA), Mhandisi Shukuru Suleiman, katika hafla iliyofanyika mjini Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ZSSF yapewa mchongo ujenzi wa nyumba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) unetakiwa kujikita katika miradi ya kujenga nyumba zenye gharama nafuu ambazo zitakodishwa na kuuzwa kwa wananchi wa kawaida wakiwamo watumishi wa serikali.

Waziri wa Fedha na Mipango, Blozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema hayo jana wakati akizungumza na watendaji wa taasisi hiyo katika ziara ya kutembelea miradi inayotekelezwa na mfuko huo ikiwamo ujenzi wa nyumba za ghorofa, Mbweni njе kidogo ya mji wa Unguja.

Alisema mfuko baada ya kutekeleza miradi mikubwa ya nyumba zenye gharama kubwa, ni wakati mwafaka wa kujenga nyumba zitakazokodishwa kwa watu wa kawaida wakiwamo watumishi wa umma ambao ni sehemu ya mfuko huo.

"Mfuko wa hifadhi ya jamii umefanya kazi kubwa katika uwekezaji wa majengo ya biashara. Kwa sasa ni vizuri kujenga nyumba zenye gharama nafuu zitakazokodishwa kwa wafanya kazi pamoja na wananchi wa kawaida," alisema.

Naye Ofisa Miradi wa ZSSF, Abdilaziz Abdalla Iddi, alisema wako katika hatua ya kufanya utafiti wa mradi wa ujenzi wa nyumba nafuu kwa ajili ya wafanyakazi na wananchi wa kawaida huko Tunguu, wilaya ya Kati Unguja.

Alisema mradi huo lengo lake ni kuwakopesha wanachama wa mfuko ambao ni wafanyakazi wa serikali kujenga nyumba zitakazowazesha kuishi na familia zao na kulipa hatua kwa hatua.

"Tumejipanga kuhakikisha tunajenga nyumba za mkopo nafuu ambazo tutawapatia wanachama wetu ambao ni wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taasisi zake," alisema.

# Shule zisizokidhi vigezo kutosajiliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema haitasajili shule iliyoko kwenye mfumo wa nyumba za makazi kutokana na kukosa vigezo.

Kaimu Mrajis wa Elimu ambae pia ni Katibu wa Baraza la Elimu Zanzibar, Thneyuu Mabrouk Hassan, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Vuga mjini Zanzibar .

Alisema serikali imekataza uanzishwaji wa shule hizo kutokana na kukosa vigezo vya ujenzi wa shule vilivyowekwa na wizara ya elimu.

Hassan alisema sababu nyingine ya kuzuiwa kwa shule hizo ni vyumba kutokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi hali ambayo inaweza kusababisha athari kwa watoto.

Alisema shule nyingi zilikuwa zikianzishwa kwa kuangalia vigezo muhimu ikiwamo umeme, maji, vyoo na sera ya elimu ya mwaka 2006 iliyotaka kila mtoto anayefika umri wa miaka minne kuanza shule.

Kwa mujibu wa mrajisi huyo, ofisi yake imekuwa ikizipitia shule zote za Zanzibar kila muda kwa ajili ya kufanya uhakiki wa sheria, sera, kanuni na miongozo ya wizara ya elimu kuona inafuatwa.

Alisema uhakiki uliofanywa mwaka 2017 kwa Zanzibar nzima, shule 99 zilibainika kutosajiliwa na kuchukua hatua ya kuzifungia.

Kwa sasa, alisema shule inayosajiliwa ni ile yenye viwango vyote vinavyotakiwa na mazingira ya Shule ambayo anataka kuianzisha.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa sheria ya elimu kipengele cha 14, shule zote zinatakiwa kusajiliwa kabla ya kuanzishwa.

Kutokana na sababu hiyo, aliwataka wamiliki wa shule licha ya kwamba wamesajiliwa katika shule ambazo majengo yake ni nyumba za makazi, kutafuta maeneo maalum ya kujenga madarasa ambayo yako katika mfumo wa shule yenye ubora unaotakiwa na wizara, ikiwamo ukubwa wa madarasa na madirisha kwa ajili ya usalama wa watoto.

KHADIJA KOPA
UKURASA 12







WAMEHEMEWA

# Mwana FA, Babu Tale wana mtihani mzito

BAADA ya Chama cha Mapinduzi, kutaja majina ya wagombea wake katika majimbo mbalimbali, majina ya Babu tale na Mwana FA, ni miongoni yaliyoleta mjadala mkali.

Mwana FA ambaye ni mwanamuziki wa aina ya Hip hop na Babu Tale ambaye ni meneja wa mwanamuziki Diamond Platnumz, sasa wataingia katika hatua ya pili ya kuwania nafasi ubunge, nayo ni kuomba ridhaa na kupigiwa kura katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba.

Baada ya kutajwa kwa majina yao, wasanii hao wameonekana kama wamehehemewa, yaani wamezidiwa na furaha na kila mmoja alitoka na jambo lake lililowashangaza wengi.

Babu tale yeye atawania ubunge wa Morogoro Kusini na MwanaFA, atapigania jimbo la Muheza.

Kutokana na kuzidiwa na maneno, kila mmoja hakuwa na kugha tamu ya kuelezea furaha yake, Mwana FA, alibaki kumtukuza Mungu, huku Babu Tale, akiangua chozi.

"Mungu ni mwema sana, Leo ni miongoni mwa zile siku chache, mimi nimeishiwa na sina la kusema, alama nyingine kuhusu ukubwa wa Mungu" aliandika MwanaFA katika akaunti yake ya Instagram.

Macho na masikio ya mashabiki wa muziki ni kutaka kushuhudia jinsi wasanii hao kama watafanya kile kinachotarajiwa endapo watapata nafasi ya kwenda bungeni.

BASI SAWA

## We Shilole unachokisema hakieleweki

MWANAMUZIKI asiyekosa vituko, Shilole, wiki hii ametoa kali baada ya kusema eti Baba Levo, amekuwa na tabia ya kuchunguza simu yake mara kwa mara ili kujua kama amepata mwanaume mwingine.

Akizungumza na EATV, Shilole amesema, Baba Levo ambaye ni rafiki yake wa karibu, mara nyingi hutumia simu yake na akishaichukua anapekuaga ujumbe wa kawaida na ujumbe wa Instagram.

"Mimi na Baba Levo tumezoeana sana, mara nyingi huwa anapoteza simu na simu yake inakuwa haina vifurushi hivyo anataka kuingia Instagram aone, kwa hiyo nikimpa simu yangu huwa anaanza kukagua ili kujua nimempata nani au wakina nani wanatuma meseji za kutaka usajili mpya, bahati nzuri sina mambo mabaya kwenye simu yangu" ameeleza Shilole




## Khadija Kopa ukongwe dawa eti!

KUNGWI lao! Ndivyo mkongwe wa muziki wa Taarab Khadija Kopa, alipoamua kujigeuza kungwi ili kuokoa penzi la wasanii nyota wa filamu nchini Chuchu Hansy na Vincent Kigosi "Ray".

Khadija Kopa, amesema anamshukuru Chuchu kutambua uwepo wake hadi kumfuata na kumuomba ushauri wake kuhusu matatizo ya uhusiano yanayomkabili.

"Ahsante mwanangu Chuchu Hans kwa kutambua uwepo wangu kutokana na matatizo yako ya kimaisha na kuja kwangu kufuata wosia wangu, Ahsante kwa kunielewa na ukayafanyie kazi, wanaume ndivyo walivyo usimalize maadam kakuomba msamaha basi huyo ni muungwana Mungu awajaalie muendelee na maisha mazuri" ameandika Khadija Kopa kupitia mtandao wa Instagram





## Madam Rita yamalize kiutu uzima

NI wazi dongo la Harmonize katika wimbo wake mpya wa 'Jeshi' limewalenga wengi. Kwani wiki hii bosi wa shindano la Bongo Star Search, Madam Rita, ameamua kujibu kwa upande wake kwa kuelezea hana tatizo na msanii huyo.

Katika moja ya mashairi ya wimbo huo, Harmonize aliwataja majaji Master J na Rita kama watu waliomuongezea bidii pale walipomkataa alipkwenda kujaribu bahati yake.

"BSS Hatuna tatizo naye, ni msanii mzuri ila kipindi kile alivyopita alikuwa hajajiandaa, sio kwamba tulimchukulia poa na tulikuwa hatumjui wala hatukumfanyia makusudi ila ni mambo ya kawaida na tunamkubali, tunafurahia anavyong'aa kwa sababu alipita pale, sekunde 30 huwezi ukaona kipaji cha mtu ila baada ya muda unaweza ukaona" amesema Madam Rita

## Karata ya Ushindi:Utamu wa muwa, vuka fundo

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote hakuna urahisi kwenye maisha. Maisha ni kama mlima kuna kupanda na kushuka. Ni kama njia ndefu ambayo ni lazima iwe na kona, miinuko na mteremko. Ni kama muwa ni lazima sehemu iwe laini, lakini unakutana na sehemu nyingine zina fundo na unakuwa mgumu na si mtamu sana.

Hii inaonyesha kuwa maisha kuna wakati yanaenda vizuri, lakini zinaweza kuja nyakati ngumu ambazo kama si mvumilivu unaweza kukufuru Mungu na kufanya uamuzi ambao si sahihi. Cha muhimu ni kuvumilia ukiomba Mungu, huku ukitafuta ufumbuzi taratibu kwa namna inayokubalika.

Tujifunze hili kupitia filamu moja inaitwa 'Karata ya Ushindi.' Imechezwa na wasanii kina Amani Almasi, Christina Januari, Zubeda Yassin, Lameck Victor, Keysha Said na Rahma Suleiman.

Inaanza kwa kuonyesha Amani akiwa anafua nguo za mkewe Tina. Mama na dada yake wanamfuata na kuanza kumpa makavu kwa nini mwanaume mzima anafua nguo za mkewe.

Wanamwambia kwa mila za Kiafrika ni jambo lisilokubalika na ni aibu kubwa kwenye familia na ukoo wao.

Amani anawaambia kuwa wasimpangie cha kufanya kwa sababu ameamua kumsaidia mkewe na alimuahidi kuwa atakuwa naye na anampenda kwa shida na raha.

Love, dada wa Amani anapita mitaani na kuwatangazia watu kuwa wifi yake ni kikojozi, anakojoa kitandani na pia anatokwa kwa haja kubwa, na kaka yake amekuwa akifanya kazi ya kumfulia nguo kila asubuhi.

Uvumi huo ukaenea kijiji kizima na ukawagawanya watu sehemu mbili. Wapo waliolifurahia na kuzidi kumcheka, kumbeza na kumtania kila anapopita, lakini wapo waliomuonea huruma na kuchukia kitendo cha watu kumcheka mtu mwenye matatizo.

Tina akawa hana raha, kila anapopita anakutana na vijembe kutoka kwa wanawake wenzake wale wasiompenda.

Kijana mmoja anamfuata Amani na kumwambia ampeleke mkewe kwa mganga wa kienyeji.

Amani na mkewe wanafanya hivyo, lakini badala ya hali kutengemaa, inazidi kuwa mbaya.

Mama mkwe na wifi yake Tina, wanaendelea kumnyanyasa mwanamke wa watu na kama Tina angekuwa na 'roho ndogo' angeondoka, lakini alimpenda mumewe. Pia kitendo cha mumewe kuwa pamoja naye licha ya matatizo yote, nacho pia kilimtia moyo.

Amani anaitwa na mwalimu wa mtoto wake shuleni kutokana na mahudhurio yake kuwa hafifu.

Lakini pia mwalimu anachukua fursa hiyo kumuuliza Amani maswali ambayo anasikia yakisemwasema mtaani kuhusu mkewe. Amani anaamua kufunguka kuwa ni kweli mkewe ana tatizo hilo.

Mwalimu anamwambia Amani kuwa mkewe hajarogwa, bali huo ni ugonjwa wa fistula, hivyo ampeleka haraka hospitali.

Amani amapeleka mkewe hospitali, anapata matibabu na anapona kabisa. Hii ikaleta furaha kwa wanandoa hao ambao walinyanyasika kwa kutosha, huku mama yake Amani na dada yake, wakipatwa na aibu iliyowafanya waombe radhi.








## Mavoko kwa sangoma ulifikaje tena?

MENEJA wa zamani wa msanii Rich Mavoko, anayeitwa Meneja Maneno, ametoa siri nzito baada ya kudai yeye na mwanamuziki huyo waliwahi kwenda kwa sangoma kusafisha nyota.

"Kwa Mganga tulienda kwa sababu zile zilikuwa mbinu za njia za kupita ili kuweza kufanikiwa, usitegemee kutuona tena kwa waganga ila tegemeeni kuona muunganiko mzuri kwetu na kumuona Rich Mavoko anakwenda sehemu nzuri, mambo mengine yote yamepita na tumeweza kusuluhisha" amesema Meneja Maneno

Aidha, Meneja Maneno amesema tatizo la wao kutofautiana lilikuwa yeye kuwa na jazba nyingi na kushindwa kusalimiana kwa muda wa miaka sita. Hata hivyo kwa sasa wapo vizuri baada ya kuyamaliza.

## MAKAMANDA WALIOZIBEBA BENDI ZILIZOWIKA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE tasnia ya muziki wa dansi, wapo wanamuziki ambao watakumbukwa kutokana na kuziongoza bendi zilizowika na kuipatia sifa Tanzania na ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati.

Mashabiki walikuwa wanakwenda kwenye kumbi za muziki wakiserebuka na wengine kuzisikiliza kwenye redio wakifurahia ufundi na upangaji mzuri wa muziki huo, pamoja na sauti za wanamuziki wenyewe.

Lakini bila kujua kuwa bila uongozi mzuri, wasingeweza kupata burudani hizo ambazo hadi leo bado zimeendelea kupendwa na mashabiki wengi, hata vijana wa kizazi hiki.

Leo tutawaangalia wanamuziki waliokuwa wakiziongoza bendi hizo ambazo zilifanya vema sana nchini Tanzania na kutetemesha eneo lote la Afrika Mashariki na Kati.

**Said Mabera-Msondo Ngoma**

Sifa kubwa apewe mwanamuziki huyu ambaye alihamia kwenye bendi hiyo mwaka 1973 akitokea Arusha, akiwa anapiga trumpet. Awali alikuwa kiongozi wa bendi wa Nuta jazz ambayo baadaye ikawa Juwata Jazz, Ottu Jazz na Msondo Ngoma Music.

Alianza kuiongoza bendi hiyo kuanzia mwaka 1978 wakati Muhidini Gurumo alipohama na kwenda kuanzisha Mlimani Park Orchestra. Ni miaka 42 sasa anaendelea kuwa kiongozi wa bendi hiyo.

Awali Abel Bathazal pamoja na Muhidini Gurumo ndiyo waliokuwa viongozi wa bendi hiyo, kabla ya Abel kuhama mwaka 1977 kwenda kuanzisha Dar International.

Mabera ni kamanda shupavu aliyeiongoza Msondo kwenye mazingira mazuri na magumu, hasa kwenye misukosuko ya mara kwa mara ya kuondokewa na wanamuziki mahiri, lakini akisimama imara na bendi kiasi cha kutotetereka, ikiwa ni moja ya bendi mbili kuu kubwa zenye mashabiki wengi nchini kama Simba na Yanga.

**Muhidini Maalim Gurumo-Mlimani Park**

Ni mmoja wa wanamuziki wenye rekodi kubwa ya muziki wa Tanzania, akiziongoza bendi zote kuu nchini ikiwamo Msondo na Sikinde. Lakini pia alikwenda kuliongoza kundi la Orchestra Safari Sound (OSS), akiasisi mtindo wa Ndekule 'ngoma ya mababu'.

Ndiye mwasisi wa mitindo ya 'Msondo Ngoma', Sikinde Ngoma ya Ukae' na 'Ndekule Ngoma ya Mababu', zote zikiwa ni ngoma za Kizaramo ambalo ndilo kabila lake la asili.

Gurumo ameyaongoza makundi haya kwa uwezo wa hali ya juu na alikuwa anasifika mno kwa kusimamia maslahi ya wanamuziki kutoka kwa waajiri. Alifariki dunia mwaka 2014.

**Nguza Mbangu Viking-Maquiz Original**

Huyu kwa sasa wengi wanamfahamu kama 'Babu Seya', kutokana na wimbo wake wa 'Seya' wa miaka ya '80, kuurudia tena kwenye miaka ya '90 na kupendwa na watu wengi.

Baada ya kifo cha aliyekuwa kiongozi na mwenyekiti wa bendi hiyo iliyotokea nchini Congo DR, wakati huo ikiitwa Zaire, Chinyama Chiyaza mwaka 1986, Nguza akachukua kijiti na kuiongoza kwa mafanikio makubwa hadi bendi hiyo ilipovunjika wakati yeye akiwa ameshahama na kuunda bendi yake binafsi.

**King Kiki-OSS Masantula**

Ni mwanamuziki ambaye kizazi cha sasa kinamfahamu kwa wimbo wake wa 'Kitambaa Cheupe'.

Ni mwanamuziki, mwimbaji na kiongozi ambaye anaheshimika na watu wote.

Inasemekana ndiye mwanamuziki aliyetokea kupendwa na kukubalika zaidi na mashabiki kuliko yoyote yule aliyewahi kutokea kwenye ardhi ya Tanzania.

Alikuwa akiingia dansini na mabaunsa, umati wa watu, joho lake likishikiliwa na akinadada warembo.

Huyu aliyaongoza makundi ya Orchestra Safari Sound akiasisi mtindo wa Masantula Ngoma ya Mpwita, King Kiki Double 0, na kwa sasa analiongoza kundi la Ya Capital Wazee Sugu.

**Fredie Ndala Kasheba-OSS Dukuduku**

Bendi ya Ochestra Safari Sound ilipitia nyakati mbalimbali, ya kwanza ilikuwa ni ya Kiki miaka ya mwanzoni mwa '80 akiita Masantula, ya pili ilikuwa ni ya Ndala Kasheba huko huko mwanzoni mwa miaka ya '80, akaiita dukuduku. Kasheba aliendelea kuifanya bendi hiyo kuwa bora na yenye ushindani wa hali ya juu, akiwa na gita lake la nyuzi 12, au dazani na kusababisha bendi nyingi nazo kuiga, kabla ya kuondoka mwaka 1985 na Gurumo kuchukua kijiti, akileta mtindo wa Ndekule.





# Churchill kama si kweli bora unyamaze

MUME wa zamani wa mwigizaji, Tonto Dikeh, Olakunle Churchill amekanusha kuwa na mtoto na msanii mwingine.

Churchill ambaye ni mfanyabiashara nchini Nigeria, amekanusha kuwa mtoto wa TBoss kuwa ni wake na kwamba uvumi huo hauna ukweli.

"Nimepata maswali mengi kuhusu kuzaa na staa Tboss' baby, ukweli ni kwamba sio wangu," amesema.




## Duh! Fuse umechoma picha ya Yesu?

STAA wa muziki wa Ghana ambaye ana makazi yake Uingereza, Fuse ODG, ameibua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii baada ya kuichoma moto picha ya Yesu.

Picha zenye uso wa mtu ambaye anaaminika kuwa ni Yesu kristo, imekuwa alama kuu kwa waumini wa dini hiyo na kitendo cha kuichoma moto inatafsiriwa kama uasi.

Kulingana na  Fuse ODG, mchoro wa Yesu unaomuonyesha ana asili ya kizungu ni ubaguzi na ni sawa na kufananisha na dikteta  au utawala wa kibaguzi uliokuwa Afrika Kusini.

## Hii hapa 'Playlist' ya Obama wasanii Afrika

IMEKUWA jambo la kawaida kwa aliyekuwa Rais Marekani, Barack Obama, kutaja wanamuziki anaopenda kusikiliza nyimbo zao.

Mwaka huu, kiongozi huyo ametoa orodha ya nyimbo ambazo anazisikiliza katika kipindi hiki cha majira ya joto.

Nyimbo hizo ni Smile' Wizkid Ft H.E.R, 'Be Honest' ya Jorja Smith & Burna Boy, 'Already' ya Beyonce & Shatta Wale na 'The Climb Back' iliyoimbwa na J cole.






## BBNaija moto, washiriki wasutana

SHINDANO la Big Brother Nigeria 2020, linazidi kunoga, mashabiki wanaolifuatilia kupitia runinga zao wanazidi kupagawishwa kutokana na vituko vya washiriki wanaoishi pamoja ndani ya nyumba.

Wiki hii, mshiriki Kiddwaya, aliamua kuomba radhi kwa wenzake baada ya kuzua tafrani kutokana na ujumbe wake.

Mwaka huu, BBNaija inafanyika ikiwa watu wapo majumbani kwao kutekeleza amri ya serikali ya kutotoka nje kwa ajili ya kukabiliana na virusi vya corona.

Ujumbe ambao Kiddwaya, alionekana kwenda kinyume na sharti hilo, lilizua mjadala ndani ya nyumba hiyo, lakini haraka aliamua kuomba radhi kutokana na usumbufu wa kile alichokisema.

## Omotola yamkuta tena

HABARI mbaya! Mashabiki wa mwigizaji mkongwe wa Nollywood, Omotola Jalade Ekeinde , wiki hii wamekuwa na wasiwasi baada ya msanii huyo kugundulika ameambukizwa virusi vya Covid 19.

Omotola, ametumia ukurasa wake wa Instagram, kuwataarifu mashabiki wake kwamba amepata vipimo vua corona na majibu yanaonyesha amepata maambukizi.

"Hello mashabiki wangu, najua mtashangazwa na haya ninayowaambia, nilikuwa naumwa na sasa naendelea vizuri na baada ya vipimo vinaonyesha nina Covid 19...lakini sasa nipo vizuri," amesema Omotola.



MAKALA

# MANDHARI MURUA

## ■Mwanga wa jua unabadilisha rangi ya anga
## ■Inapendezesha muonekano wa alfajiri na jioni

FIKIRIA pale unapoamka majira ya alfajiri na kushuhudia anga likiwa na rangi tofauti ambayo inakuvutia machoni.

Macho yako yatapambana na muonekano wenye rangi ya chungwa, zambarau au nyekundu yenye udhurungi pale jua linapochomoza asubuhi au machweo ya jioni.

Hakika ni mandhari inayopendeza, mara nyingi katika nyakati hizo watu hupumzika na kufurahia mabadiliko haya ya kiasili.

Lakini sio wengi wanajua kwa nini mabadiliko haya ambayo pia hulifanya jua kuwa na rangi jekundu au chungwa.

Mabadiliko hayo hayaji hivi hivi, bali inatokana na matokeo ya fizikia katika mfumo wa jua kuifikia Dunia.

Kulingana na mtaalamu wa fizikia, Edward Bloomer, kutoka makumbusho ya Royal Greenwich, ni kwamba mabadiliko hayo ya anga yanajulikana tangu siku nyingi, yote hayo yaligundulika zamani.

Anasema, kwanza tunahitajika kuelewa kwamba mwanga umetengenezwa kwa mpangilio wa nuru wenye rangi nyekundu, chungwa, kijani, samawati na zambarau.

"Hapa inahusisha mwanga uliotawanyika na kila mtawanyiko hauna usawa," anasema Bloomer.

Kila rangi ina kiwango cha wimbi lake, na hapo ndipo hufanya kila rangi huonekana ilivyo.



Muonekano wa anga katika nchi za Savanna

Kwa mfano, mwanga wa rangi ya zambarau una wimbi fupi ukilinganisha na rangi nyekundu.

Hatua nyengine ni kuelewa kuwa anga lina matabaka ya gesi. Moja ya gesi hiyo Oksijeni ambayo tunayotumia kupumua.

**KUTAWANYIKA KWA MWANGA**

Wakati mwanga unapopita matabaka tofauti angani, kila moja ikiwa na gesi ya uzito tofauti, unapinda na kugawanyika kana kwamba unagonga kwenye mche.

Mwanga huo unapopita kwenye matabaka, kuna chembe ambazo zinafanya kugawanyika na kisha kugonga na kuakisiwa.

Wakati jua linapochomoza au linapotua, miale yake inapiga tabaka la juu la anga katika muonekano wa pembe, hapo ndipo miujiza inapoanza rasmi.

Miale ya jua huchoma matabaka ya juu na hapo mwaga wa samawati hugawanywa na kuakisiwa badala kunyonywa.

"Jua linapokuwa chini kwenye upeo wa macho, rangi ya samawati na kijani hutawanyika, na hapo hupatikana rangi ya chungwa na mng'ao fulani wa rangi nyekundu," anafafanua Bloomer.

Mabadiliko hayo inapatikana kwa sababu mwanga wa umbali mfupi wenye rangi ya zambarau na samawati hutawanywa zaidi kuliko mwanga wa umbali mrefu ya machungwa na nyekundu.

Katika mtawanyiko huu wa mwanga unasababisha uwepo wa rangi za kuvutia katika anga.

Kukiwa na mchanga kwenye anga, unaweza kuona anga la rangi ya waridi na nyekundu mfano wa sayari ya Mahiri

Wakati kunakuwapo na muonekano huo wenye manthari nzuri, lakini jua halibadiliki.

Hata hivyo, rangi hizo za kupendeza inategemea sehemu ulipo duniani, anga yenu inaweza kuwa na muonekano mzuri zaidi kuliko sehemu nyingine.

"Mawingu ya vumbi, moshi na vingine kama hivyo vinaweza kuathiri muonekano wa anga pia," amesema mtaalam huyo.

Kwa mfano kama unaishi India, California, Chile, Australia au maeneo mengine ya Afrika au karibu na mchanga mwekundu, mazingira yanaweza kuwa mazuri na akisi ya mwanga ikitegemea na hali ya hewa.

"Inaweza kuwa kama inavyotokea kwenye sayari ya Mars, pale vumbi jekundu linapokuwa kwenye anga, itatoa muonekano kwamba anga ni jekundu hivi na rangi ya waridi," anazidi kusema.

Kwanini hili linatokea?

Hatua ya amri za kutotoka nje katika mataifa mengi, imefanya watu kupata fursa ya kutazama uhalisia wa dunia kwa karibu zaidi.

"Kipindi chote cha watu kufungiwa kwa kwa sababu ya corona watu wamekuwa wakishuhudia hali hiyo, pengine kwasababu hakuna cha zaidi kinachoweza kufanywa!" anasisitiza katika maoni yake.

Jua likiwa juu kwenye anga, mwanga wake unapita kwenye anga bila kugawanywa, na unanyonywa kadiri unavyoendelea kujitokeza na kuonekana kwa rangi ya samawati.

Lakini bila shaka, mambo yanaweza kubadilika ikitegemea na hali ya anga.

Ikiwa kutanyesha mvua huku jua linawaka, kisha mwanga unagawanywa kwa umbali tofauti na kila tone la mvua, na matokeo yake ni mwanga wa rangi zote kutawanyika kwenye anga. Hapo ndipo utaona upinde wa mvua ukijitokeza.



Muonekano wa anga katika jangwa la Sahara

# Wadau nishati jua wanavyoigeuza taaluma mlango kuajiri mamia nchini

## ■Mbinu gani? Wataja kuziba mapengo 6
## ■Cherehani, vinyozi, vibanda vya video

**Na Beatrice Philemon**

LEO, ni siku kuu kwa wadau wakuu asasi ya Sepon inayohimitisha miaka saba kutoa huduma hiyo kitaifa. Nipashe ilizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wake, Bernard Okech, kudadisi mchango wao katika eneo hilo la nishati wanayowahudumia Watanzania na maisha yao. Fuatilia mazungumzo yao':

**SWALI:** Wakati mnatimiza miaka saba ya kuwapo nchini, unaweza kutaja yapi ya mafanikio katika miaka hii mitano inayotimu sasa, kuwapo kwenu nchini?

**JIBU:** Sepon iliunda programu iitawayo 'Solar Mtaji' iliyozipa uwezo biashara ndogo na zikawezeshwa nguvu za kutosha na kufungua fursa za ajira kwa vijana na kinamama wa Kitanzania. Muundo wa biashara hii imetuwezesha kuhudumia wateja 380, wanaiona asasi ya Sepon inajaili ustawi wao.

Kwa maana hiyo, tukaingiza nishati jua katika cherehani (katika huduma za ushonaji), vinyozi, kumbi za televisheni wanakoonyesha mechi za mpira, kuchaji simu za mkononi kwa malipo maalum, vituo vya Tehama vijijini kutoa nakala, kudurufu, kufanya 'scanning', kutuma baruapepe na huduma nyinginezo za kidigitalii katika maeneo ya vijijini hususan (mikoa) Dar es Salaa, Kagera, Pwani na mikoa mingine.

**SWALI:** Kwa kifupi, unaweza kutoa historia ya asasi ya Sepon?

**JIBU:** Kampuni ya Sepon ilianza kazi Agosti 22, mwaka 2013 katika ofisi ndogo yenye ukubwa wa upana mita 12 kwa mbili eneo la Sinza Mori Dar es Salaam, ikiwa na mkurugenzi mtendaji na ofisa utawala, ndio timu kamili ya watumishi.

Taasisi iliundwa kutoa huduma bora ya bidhaa ya nishati endelevu na kuwahudumia umma wa walio maeneo ya mijini na vijijini, Sepon ilianza na taa za nishati jua na ikakua hadi kufikia biashara ya kutoa mfumo wa nishati jua kwa asasi tofauti za Tanzania Bara na Zanzibar.

Kampuni ilianzishwa na Benard Okech na mke wake, Ester Sommy na mwanafunzi mwenza wa darasa moja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliosoma MBA (Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara), Chesco Charles Mwepelwa.

Ni mapengo ambayo Benard aliyaona katika asasi za kuhudumia nishati jua katika miaka yake sitaya kuajiriwa kwenye sekta ndogo ya nishati jua ndani ya Afrika Mashariki.

Kwa mfano, alithibitisha kampuni nyingi hazikuwa zinatoa huduma bora baada ya kufanya mauzo na hapo ndipo kampuni ya Sepon iliamua kuziba pengo, kuhakikisha wateja wanaridhishwa na huduma, baada ya kuwawekea




Kikundi cha mfano, kinamama mafundi cherehani wanaotumia nishati jua, Magomeni, Dar es Salaam.
**PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

huduma na baada ya kufungha mitambo hiyo.

Mkakati uliwezesha kampuni kupata wateja wengi, kwani walimiminika na kuazisha kampuni kupanua huduma zake kwingine nchi nzima, Bara na Visiwani.

Pili, matumizi ya nishati jua hayakusisitizwa na asasi nyingi, pindi tu Mpango wa 'Solar Mtaji; ulipoanzishwa na Sepon.

SWALI: Unaelezaje sekta ya nishati jua ilivyo nchini Tanzania?

JIBU: Gharama ya nishati jua kwa miaka saba inazidi kushuka, ikikaribia na tozo la nusu gharama ya mwaka 2013. Hata hivyo, kutokana na ongezeko la bati katika soko la kimataifa, gharama ya betri nayo inapanda kila mwaka

Hivyo, tulichofanya kampuni ya Sepon ni kurekebisha mifumo ya nishati yetu iendane na mabadiliko katika soko la kimataifa, pia kuwafanya wateja wamudu soko.

**SWALI:** Ni mabadiliko gani umeyashuhudia katika sekta ya nishati jua kwa miaka hii saba na katika mtazamo wako, upi mwelekeo wa sekta?

**JIBU:** Kutokana na maboresho mbalimbali, yaliyofanyika katika miaka saba iliyopita, teknolojia ya nishati jua ndio dira yetu kwa sasa inayosaidia kuwezesha maendeleo ya viwanda na matumizi katika uzalishaji katika biashara mbalimbali. Ndio mwelekeo wa nishati jua na si matumizi ya nyumbani pekee.

Matumizi ya uzalishaji yanafungua ajira mpya kwa vijana na kinamama na inawezesha taasisi mbalimbali na biashara zao kukua.

Hiyo ndio sababu kampuni ya Sepon inajikita katika mpango wa 'Solar Mtaji' katika sehemu mbalimbali za nchi nishati jua itumike katika biashara za vijijini kuwafungulia ajira, vijana, kinamama na mijini na vijijini.

**SWALI:** Namna gani Watanzania wanaichukulia nishati jua na namna ninyi kampuni ya Sepon mnafanyia kazi mtazamo wao?

**JIBU:** Mwanzo, nishati jua ilichukuliwa na Watanzania wengi kuwa matumizi ya nyumbani na kwa ajili ya vifaa vidogo pekee. Kwa mengi yaliyofanywa na Sepon kuonyesha kwa mifano sokoni kwamba ina uwezo kamili wa matumizi ya uzalishaji.

Wateja wetu wanatumia jua kuendesha biashara zao katika sehemu tofauti ya Tanzania. Imethibitisha kwamba nishati jua inaaminika, endelevu na inaokoa gharama za matumizi kwa kuwezesha uongezeko la faida

Kwa mfano, kikundi cha kinamama cha Magomeni, jijini Dar es Salaam, kinachotumia nishati jua kwa ajili ya kuendesha cherehani, hata imewawezesha kuhudumia nguo za ziada 20 na kuwaongezea shilingi 200,000 kwa siku, ikawawezesha kuongeza mitambo ya nishati hiyo.

Hii ina maana kuwa kikundi cha kinamama saba mafundi nguo, wanaingiza shilingi milioni tano kwa mwezi, ikilinganishwa na gharama ya Sh. milioni tatu walizotumia kuwekeza mifumo hiyo ya jua

**SWALI:** Nini dira ya kampuni ya Sepon na mnakolenga ifikie katika miaka 10 ijayo?

**JIBU:** Kutokana na matokeo makubwa chanya ya mpango wa 'Solar Mtaji' wenye matokeo chanya ya kiwango kikubwa, lengo kuu ni kuvifikia vituo 10,000 vya kibiashara vyenye huduma bora na kuzalisha ajira 20,000 katika miaka 10 ijayo na kuwezesha kipato cha uhakika kwa Watanzania 100,000 wenye mazingira salama.

Kwa kuwa wateja hupenda kuafahamisha ndugu na marafiki. Tunatarajia wateja wanaoridhika watatuletea mara tatu ya matokeo chanya ya sasa na kuifanya asasi ya Sepon kuwa ya mageuzi, nchini Tanzania ndani ya miaka 10 ijayo, hatimaye Afrika Mashariki yote.

Hitaji letu ni kuona wale wenye utashi wa kusimamia gharama zao katika biashara, vijijini na pembezoni mwa miji, wanawasiliana nasi kwa ajili ya namna ya kupunguza gharama hizi ili wapate mageuzi wanayonuia.

**SWALI:** Ni Watazana watarajie kutoka kampuni yako kwa sasa?

**JIBU:** Mwaka 2020, Sepon inatarajia kuhudumia biashara ndogo walau 100, kwa kuwapa nishati jua katika vituo vyao kwa thamani ya Sh. milioni tatu kila kimoja; vinyozi Sh. 2,700,000; kumbi za video (televisheni) kunakoshuhudiwa soka na kuchaji simu kwa Sh. milioni mbili kila kimoja.

Vivyo hivyo, tunalenga umeme jua kwa vijiwe vya Tehama vyenye biashara kamili zikiwamo mashine za kudurufu, kuchapisha, 'ku-scan', kuhudumia kompyuta mpakato; na miradi ya mafunzo ya komyuta, zikipata nishati hiyo kwa saa 12 kwa gharama ya Sh. milioni 15 tu (za uwekezaji) na aina zote za huduma za kidigitali mijini na pembezoni mwa mijini

**SWALI:** Nini kilikufanya ukaingia katika ajira ya kuhudumia sekta hii ya nishati jua?

**JIBU:** Wakati nasoma Shahada ya Sayansi, katika Chuo Kikuu cha Kenyatta (Kenya), nilijifunza mionzi Fizikia ya Mazingira kama sehemu ya mafunzo. Baada ya kuhitimu mwaka 2007, nikaanza kufanyia kazi na kuvutiwa na nishati jua katika uhalisia wake.

Tangu wakati huo, nimekuwa nikipenda teknolojia ya jua na mara nyingi nilipata fursa za kufanya kazi ya teknolojia hiyo kwa wateja kuboresha maisha yao ya kila siku, hali kadhalika shughuli za biashara.



Wahandisi kutoka kampuni ya Sepon, wakiwa kazini mkoani Kagera, kuweka mitambo ya umeme jua

HABARI KIMATAIFA

# Jeshi Mali lasisitiza kuunda serikali

**BAMAKO, Mali**

VIONGOZI wa mapinduzi nchini Mali, wametangaza wanataka kuunda serikali ya mpito haraka, huku wakisema Rais wa mpito atachaguliwa kutoka ndani ya jeshi au raia.

Mapinduzi hayo yaliyotokea siku ya Jumanne, yalisababisha kiongozi wa nchi hiyo, Ibrahim Boubacar Keïta, kutangaza kujiuzulu baada ya kuwekwa kizuizini.

Hata hivyo, viongozi wa Afrika Magharibi waletoa wito wa kuachiwa huru na kurejeshwa madarakani kwa rais huyo haraka madarakani.

Hata hivyo, jeshi ambalo limefanya mapinduzi hao walisema wanawasiliana na upinzani na makundi mengine kujaribu kuhakikisha serikali ya mpito inapatikana.

Walisema katika taarifa yao kuwa uchaguzi utafanyika wakati unaofaa na pia waliahidi kuheshimu makubaliano ya kimataifa juu ya kukabiliana na makundi ya jihadi.

Jumuiya ya Uchumi ya Afrika Magharibi (Ecowas) ilitoa taarifa ya kutuma ujumbe wake ili kuhakikisha nchi hiyo inarejesha na kufuata katiba yake.

Tangu kufanyika kwa mapinduzi hayo, wanajeshi wameongezwa nje ya wizara za serikali katika mji mkuu Bamako, lakini maduka na biashara zikiendelea.

**BBC.**



Wafanyakazi wa idara ya misitu wakimbeba chui ambaye alivamia makazi ya watu eneo la Shadnagar, tukio hilo limetokea juzi kilomita zaidi ya 60 kutoka mjini Hyderabad nchini India..**(PICH:AFP)**

# Biden amshambulia vikali Trump

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEWA wa Urais wa Marekani, kupitia chama cha Democratic, Joe Biden, alimshambulia Donald Trump, akisema ameiweka nchi hiyo katika giza kwa muda mrefu

Akiungumza wakati akikubali kuteuliwa kwake kupeperusha bendera ya chama hicho katika mkutano mkuu, Biden alisema Rais Trump amesababisha hasira, hofu na mgawanyiko miongoni mwa Wamarekani. Anaelekea kwenye kampeni za uchaguzi mkuu akiwa anaongoza kwa kura za maoni dhidi ya Rais Trump

Kwenye mkutano huo uliofanyika mjini Wilmington, Biden, (77), alisema yeye ndiye mtu anayeweza kubadilisha hali hiyo ili kila mtu afaidi matunda ya taifa hilo.

"Ninawaahidi, ikiwa mnaniamini kwa kunipa jukumu hili la urais, nitahakikisha sisi tunakuwa bora zaidi.Nitakuwa mshirika wa nuru, na si giza," alisema.

Aliongeza "Ni wakati wetu wa kuwa pamoja na kuhakikisha hatufanyi makosa, kwa kungana tunaweza na tutapambana na msimu huu wa giza Marekani,".

Hata hivyo, aliwataka wamarekani kuchagua matumaini dhidi ya hofu, uhalisia kuliko mambo ya kufikirika na haki kuliko upendeleo.

"Tunaweza kuchagua njia ya kuwa na hasira zaidi, isiyo na matumaini na iliyogawanyika," alisisitiza Biden.

Alisema watu wa nchi hiyo wanaweza kuchagua njia tofauti na wote kwa pamoja wakatumia fursa hiyo ili kupona.

"Huu ni uchaguzi wa kubadili maisha. Hii itatupa mwanga wa namna Marekani itakavyokuwa kwa muda mrefu." Aliwaambia wafuasi wa chama hicho.

**BBC**

# Macron, Merkal waomba suluhu Belarus

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amependekeza Umoja wa Ulaya na Urusi zisaidie kuutafutia ufumbuzi mgogoro wa nchi ya Belarus.

Pendekezo hilo alilitoa wakati wa mazungumzo yake ya Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, yaliyofanyika majuzi kusini mwa Ufaransa.

Rais Macron na Kansela Merkel, waliweka imani yao kwa Umoja wa Ulaya unaweza kujaribu kuwa msuluhishi wa kumaliza mgogoro huo wa kisiasa uliosababishwa na matokeo ya uchaguzi ambayo yalimpa ushindi Rais Alexender Lukashenko.

Kiongozi huyo wa Ufaransa, alisema wananchi wa Belarus wanapaswa kutafuta suluhisho, lakini alisisitiza Urusi inatakiwa kushirikishwa kwenye mazungumzo.

**DW.**

# Israel, Wapalestina warushiana roketi

TEL AVIV, Esrael

JESHI la Israel limesema roketi 12, zimerushwa kutoka katika eneo la Ukanda wa Gaza, na nane kati ya hizo zimezuiwa.

Kufuatia kitendo hicho jeshi hilo nalo lilijibu kwa kufanya mashambulizi matatu ya anga, yakilenga maeneo ambayo yanauhusisha utawala wa kundi la Hamas.

Kwa mujibu wa polisi wa nchi hiyo, majibizano hayo ya silaha yalikuwa makali zaidi kutokea katika eneo la Gaza katika miezi ya hivi karibuni.

Lakini hadi sasa haijatolewa idadi ya watu waliokufa au kujeruhiwa, ingawa majengo na magari kwa upande wa Israel yaliharibika.

Katika siku za hivi karibuni, makundi yenye uhusiano na Hamas, yalirusha maputo yaliyo na vifaa vya mripuko upande wa Israel kwa lengo la kuishinikiza nchi hiyo kuondoa vizuizi vilivyowekwa ukanda wa Gaza.

Mashambulizi ya sasa ya rekoti yanaonaongeza hofu ya kungezeka machafuko katika eneo hilo.

**DW.**

HADITHI

# Mauaji Harusini-26

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.


Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**




"Nakupenda sana Shani."

"Ahsante sherry, nafurahi kusikia hivyo. Unajua wewe umekuwa sehemu kubwa sana ya furaha yangu hivi sasa."

"Hata wewe pia umenifanya niwe na furaha zaidi, nyumbani na hata kwenye mishemishe zangu.

Ni hivi Shani, nakupenda sana kuliko neno lenyewe. Na nitaendelea kukupenda siku zote. Sikutokukwaza na sipendi kukuona huna furaha. Nitahakikisha nakulinda, uwe na afya, furaha na amani kwa sababu wewe ndiyo faraja yangu. Eddy alisema huku akiteremka kwenye gari na simu yake sikioni.

"Hata mimi nahitaji kukukumbatia, kukubusu, na kukupa maneno matamu, ulale kwenye miguu yangu, nikudekeze, unidekeze, nipate joto lako. Ahsante sana love, nenda kale sasa." Ilikuwa sauti tamu ya Shani ilisikika masikioni mwa Eddy.

Maneno matamu, kutoka kwa msichana mdogo mbichi ambaye kwa sasa alimuona ameanza kuchamka na kujiamini kuliko ilivyokuwa mwanzo, yalimfanya Eddy kufikiria kuongeza nguvu ya kuendelea kuwa naye kama mpenzi, kumfahamu zaidi.

Kichwani alijua pamoja na ambo ya mapenzi, lakini msichana huyo alikuwa na mambo mengi kichwani yanayomtatiza kama alivyomwambia mwenyewe.

"Usinione hivi Eddy, mimi nimekuwa na matatizo makubwa. Na hadi leo bado nina matatizo makubwa. Na sikuwa na mtu yoyote wa kushea naye matatizo yangu. Wewe ni rafiki yangu, naomba tuwe pamoja kwenye furaha na matatizo yangu." alilia Shani.

"Najua. Najua Shani. Tutakuwa wote. Sitokuacha peke yako. Ila kuna siku ningependa uniambie matatizo yote yaliyokupata huko nyuma, yaliyokuwepo na ambayo unaona kama yatakuwa kikwazo kwako."

"Nitakwambia, lakini siyo hapa. Nitakwambia sehemu maalum. Tukiwa wawili tu.

Alikumbuka naneno hayo aliyoambiwa walipokuwa ABC Hotel.

Ndipo Eddy alipokumbuka kuwa jioni ya siku hiyo ilikuwa ni siku ya kwenda kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kuchukua majibu ya vipimo vya chakula aliachokichukua ABC Hotel, ambacho yeye alikuwa akikitilia shaka kutokana na kwamba mletaji wa msosi huo aliokuwa akiletewa Shani, aliangusha kifuko cha sumu.

***********************************

Akiwa kwenye kiti chake cha kuzunguka, Mkemia Mkuu wa Serikali alishusha mawani yake ya macho chini na kumtazama kwa makini Eddy, aliyekuwa amekiti kwenye kiti cha wageni.

Mkononi alikuwa ameshikilia karatasi. Ilikuwa ni baada ya kusalimiana.

"Bwana Eddy, leo ndiyo siku ile ambayo nilikwambia kuwa nitakupa majibu ya matokeo ya vipimo vya mabaki ya chakula ulichotuletea." Alisema na kumeza funda moja la mate.

Eddy hakujibu kitu. Kiu yake ni moja tu. Kujua majibu hayo. "Ni kwamba mabaki ya chakula yamekutwa na akina fulani ya sumu ambayo huua taratibu. Wataalam walipima wameniambia kuwa humuua binadamu kwenye afya njema, baada ya miezi mitatu mpaka sita, kutegemea na nguvu au kinga za mwili alizonazo." Mkemia Mkuu aliongea kwa sauti ya taratibu.

Alichotarajia sicho. Mkemia alidhani kuwa Eddy angepigwa na mshangao. Badala yake kwa mbali aliona tabasamu. Hata hivyo alibaini halikuwa halisi.

"Nadhani hapo sisi tumemaliza kazi yetu, si kazi yote kuhoji kuna nini, nani ameweka, au imekuwaje." Alimaliza Mkemia.

Hakutaka kuleta sumu aliyoiokota ili wathibitishe kama ndiyo hiyo au hapata. Alichotaka kujua kama chakula alicholetewa Shani siku ile kilikuwa na sumu tu basi.

Mwenyewe aliishajua kuwa kwenye kifuko kile cha nailoni kulikuwa na sumu iliyoangushwa na mhudumu wa kiume, ambaye kwa mujibu wa Diana, alipata jina lake kuwa anaitwa Fikiri.

"Ahsante mheshimiwa, nashukuru, nilikuwa nahitaji majibu tu, mengine sasa yanahusu idara yetu, au Jeshi la Polisi." Alisema Eddy akinyanyuka, na kuagana na mwenyeji wake kwa bashasha, akarudi ofisini.

Ni dhahiri sasa kuwa kijana yule aliyeambiwa kuwa anaitwa Fikiri ndiye mhusika. Ndiye aliyeweka sumu kwenye chakula ambacho Shani ilibidi ale.

"Nia yake ni nini?" Alijiuliza "Afe" Alijijibu mwenyewe. "Lakini kwa nini afe?" Alijiuliza swali lingine.

"Msichana mrembo mwenye umri wa miaka 23 tu, kwa nini auawe kwa sumu? Amefanya nini?" Amemkataa mwanaume? Amechukua mume wa mtu?" Yote hayo yalikuwa kichwani mwa Eddy.

"Kwa nini Fikiri atake kufanya hivi? Ni yeye ndiye mgomvi wa Shani, au ametumwa tu kufanya hivyo?" Bado maswali yaliyokuwa na majibu yalizidi kumzonga.

"Ina maana kukosa mimi yule msichana angekula kile chakula baadaa ya miezi mitatu au sita angefariki dunia. Amefanya nini? Nani yupo nyuma ya mpango huu? Fikiri?" Eddy alizidi kuwaza.

Hata hivyo akili yake haikumtuma kabisa kuwa mhudumu yule atakuwa ndiye mhusika mkuu. Alidhani kuwa alitumwa. "Atakuwa ametumwa tu yule. Lakini na nani? Na kwa sababu gani? Kwa nini Shani auawe?"

Ndipo Eddy alipokumbuka maneno ya Shani kuwa ana matatizo makubwa ambayo alihitaji kumsimulia.

"Usinione hivi Eddy, mimi nimekuwa na matatizo makubwa. Na hadi leo bado nina matatizo makubwa. Na sikuwa na mtu yoyote wa kushea naye matatizo yangu. Wewe ni rafiki yangu, naomba tuwe pamoja kwenye furaha na matatizo yangu.

Nitakwambia, lakini siyo hapa. Nitakwambia sehemu maalum. Tukiwa wawili tu."

Anachojua yeye kuwa Shani ni msichana ambaye amejikuta amepoteza wazazi wake wote wawili. Baba yake ni tajiri, hivyo Shani anatarajia kurithishwa mali zote za baba yake. "Je kuwa wafanyabiashara wakubwa waliokuwa washirika wa baba yake ambayo baada ya kumuua Patiyo, wanataka wamteketeze na binti yake wa pekee? Je kwa nini wasitumie bastola kama walivyomuua baba yake tajiri na mwenye ulinzi ambaye wamemuua 'kitemi' zaidi, kwa nini watake kumuua binti mnyonge asiyekuwa na uwezo wowote hata wa kujilinda kidhaifu na kwa woga zaidi?" Eddy alichanua mambo na akili yake ikamwambia kuwa huenda waliomuua baba yake Shani, aitwaye Patiyo na mkewe waliokuwa wakitoka kufunga naye ndoa, ambaye Eddy alikuwa ni Shangazi yake aitwaye Grace, si watu walewale.

Kitu cha kwanza alichoona kinaweza kumfanya apate mwanga zaidi ni kuonana na Fikiri kwanza.

"Ndiyo. Yeye ndiye atasema nani aliyemtuma na ndiye atatoa mwanga kama ni yeye mwenyewe ndiye alitaka kufanya hivyo au la." Kitu kimoja ambacho Eddy hakutaka kufanya ni kumfahamisha Shani kuhusu jaribio lake la kutaka kuuawa kwa sumu. Hakutaka kwa sababu ingemtisha na kuanza kuishi kwa wasiwasi.

Alitaka kwanza ajue kwa nini na ni nani aliyefanya vile, amtie mbaroni ndiyo Shani afahamu njama hizo.

"Ni lazima nimkakamate mtu huyu anayetaka kumuua mpenzi wangu. Na inawezekana ikawa ni chanzo cha kujua juu ya kifo cha shangazi yangu Grace na mumewe Patiyo waliuawa masaa kadhaa baada ya kutoka kufunga ndoa." Eddy aliapa.

***Itaendelea Jumamosi***

## HABARI KITAIFA




Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, Msekeni Mkufya (kulia), akikabidhi kwa Anthony Mavunde fomu ya uteuzi ya kugombea ubunge wa jimbo hilo, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), jana. **PICHA: IBARAHIM JOSEPH**

# Jafo afichua siri shule za serikali kung'ara kidato 6

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Selemani Jafo, ametaja sababu ya kung'ara kwa shule za serikali katika matokeo ya mtihani wa kidato cha sita mwaka huu.

Katika matokeo hayo yaliyotangazwa jana visiwani Zanzibar na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), shule nane kati ya 10 bora kitaifa ni za serikali.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dodoma jana muda mfupi baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo, Jafo, alisema mafanikio hayo ni matokeo ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ya awamu ya tano katika sekta ya elimu nchini.

Alisema matokeo hayo yameonyesha pia katika shule hizo nane za serikali zilizoingia 10 bora, tatu zina asili ya shule za kata.

"Kutokana na uwekezaji uliofanywa na Rais John Magufuli, tulipanga ifikapo mwaka 2020, shule sita ziwe zimeingia kwenye kundi la 10 bora. Leo (jana) nina furaha kubwa kuwajulisha kwamba tumevuka lengo na zimeingia shule nane badala ya sita," alitamba.

Alisema katika matokeo yaliyotangazwa jana, ufaulu umeonekana kupanda kutoka asilimia 98 hadi na kufikia asilimia 99.5.

"Wanafunzi waliopata ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu ni asilimia 97.74. Haya ni mafanikio makubwa, malengo yetu yalikuwa kuingiza shule sita za serikali kwenye 10 bora, lakini tumeingiza shule nane," alisema.

Waziri huyo alisema upande wa kidato cha kwanza hadi cha nne, matokeo ya uwekezaji uliofanywa yataanza kuonekana mwaka 2022.

Alisema ndani ya miaka mitano, kiasi cha Sh. trilioni 1.09 kimetolewa kwa ajili ya kugharamia mpango wa elimumsingi bila malipo na kiasi cha Sh. bilioni 588 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule.



Ofisa Msaidizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jimbo la Amani, Rukia Mkali Fadhil (kushoto), akimkabidhi Maalim Juma Hassan fomu ya uteuzi wa kugombea ubunge wa jimbo hilo, kupitia CCM, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aliyeanguka CCM achukua fomu ACT

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

ALIYEWAHI kuwa Mbunge wa Dodoma Mjini (2010-2015) kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), David Malole, amechukua fomu ya kuomba kuteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuwania ubunge wa jimbo hilo kwa tiketi ya chama cha ACT-Wazalendo.

Malole ambaye pia alishindwa kura za maoni ndani ya CCM kuwania jimbo hilo, amebadili gia na kuchukua fomu kupitia chama hicho jana na kukabidhiwa fomu na Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, Wakili Msekeni Mkufya.

Akizungumza mara baada ya kuchukua fomu, Malole alisema ameamua kwenda upinzani kwa kuwa CCM haimtaki.

"Nilipogombea Uenyekiti wa Wilaya ya Dodoma, niliandika barua ya malalamiko kwa Katibu wa Mkoa na Taifa CCM, mwisho wa siku niliandikiwa barua ya kalipio nisigombee kwa miaka miwili nafasi yoyote ndani ya CCM.

"Nilifikiri mzaha, ilipofika kwenye uchaguzi huu nilichukua fomu kuomba kuteuliwa ndani ya chama, lakini sikushinda, nikaona hawanitaki," alisema.

Kada huyo mpya wa ACT-Wazalendo alisema kuwa akipata ridhaa ya kuwa mbunge, atahakikisha anashughulikia kero ya ardhi ili wazawa wasinyanyaswe na pia kuboresha huduma za elimu, afya na barabara.

**"Nilipogombea Uenyekiti wa Wilaya ya Dodoma, niliandika barua ya malalamiko kwa Katibu wa Mkoa na Taifa CCM, mwisho wa siku niliandikiwa barua ya kalipio nisigombee kwa miaka miwili nafasi yoyote ndani ya CCM**




# JIMENEZ

## PATINA MZURI WA RONALDO- CAPELLO

**TURIN, Italia**

RAUL Jimenez ni "patina sahihi" kwa nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo, kwa mujibu wa Fabio Capello.

Nyota huyo wa Wolves, amekuwa akihusishwa na kujiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, baada ya kufunga mabao 27 katika mechi 55 msimu wa 2019-20.

Capello anaamini mchezaji huyo wa kimataifa wa Mexico, anaweza kuwa na kile alichokuwa akikifanya Karim Benzema kwa upatina mzuri na Ronaldo pale Real Madrid.

"Tatizo la Juve ni kwamba wanatakiwa kuuza wachezaji na kuwatoa wengine halafu kuingia tena sokoni," alisema kocha huyo wa zamani wa Juve na Madrid akinukuliwa na ESPN.

"Nimemuona Raul Jimenez, yeye ni mchezaji muhimu ambaye ana ubora wa kutosha.

"Ni mchezaji anayefaa kuc pamoja na Cristiano Ron kwa sababu Cristiano ame kile kitu alichokuwa akikipata kutoka kwa Benzema hapa Juventus. Na Raul Jimenez anaweza hilo."

Ronaldo amefunga mabao 37 katika mechi 46 msimu wa 2019-20, lakini Juve ilitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora kabla ya Maurizio Sarri kufukuzwa.

RAUL Jimenez

## VERRATTI YUPO TAYARI KUIVAA BAYERN

**LISBON, Ureno**

MARCO Verratti amesema atafanya kila kitu kuichezea Paris Saint-Germain kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich, mechi ambayo ameielezea kuwa ni dakika 90 muhimu zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Italia, Verratti hakuweza kucheza kwenye hatua ya robo fainali ya ushindi dhidi ya Atalanta kutokana na kuumia kigimbi cha mguu.

Verratti aliingia kwa muda mfupi wakati PSG ikiifumua RB Leipzig na kutinga fainali itakayopigwa Jumapili hii katika dimba la Estadio da Luz.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anafanya kila linalowezekana ili kuwapo kwenye mchezo huo, ingawa uamuzi wa mwisho upo chini ya kocha, Thomas Tuchel.

Alisema: "Nina furaha hapa, nilianza tena taratibu na timu. Majeruhi haya kwa kiasi fulani yalikuwa magumu kwangu. Nimeweza kurudi kwenye mazoezi na timu siku mbili au tatu zilizopoita na nitafanya kila kitu kucheza mchezo huu.

"Nilikuwapo kwenye nusu fainali. Ni kocha ndiye atakayefanya uamuzi wa mwisho."

## WAKALA WA NEYMAR AMVUTA MESSI, CR7 PSG

**PARIS, Ufaransa**

WAKALA wa Neymar ameshauri kwamba, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo wanatakiwa kumfuata nyota huyo wa Brazil kule Paris Saint-Germain.

Majaliwa ya Messi yako shakani baada ya Barcelona kufumuliwa mabao 8-2 na Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia kumekuwa na uvumi kwamba Juventus inaweza kuangalia kumuuza Ronaldo, ambaye ameshinda mataji mawili ya Serie A katika misimu miwili pale Turin, lakini akishindwa kuwapa furaha kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi kwa miamba wa Hispania, Barca au Real Madrid na wakala wake, Wagner Ribeiro amebainisha alifikiria kuhusu uhamisho huo.

Hata hivyo, sasa anajiamini kwamba mshambuliaji huyo atabaki Ufaransa hadi angalau mwaka 2022 na anafikiria Messi na Ronaldo wanaweza kujiunga naye pale Parc des Princes kama wamiliki wa PSG kampuni kutoka nchini Qatari wataweka fedha mezani.

"Kuna wakati alikuwa na huzuni kwa sababu ya kuwa majeruhi," alisema Ribeiro akiiambia Placar.

"Muda ule, alikuwa tayari kuondoka, kurudi Barcelona au kwenda Real Madrid. Lakini si leo unaweza kuona namna gani alivyo na furaha.

"Neymar ana furaha na anafikiri atabaki PSG kwa angalau miaka miwili zaidi. Leo bila shaka yoyote, ni rahisi kwa Messi kwenda PSG kuliko Neymar kurudi Barcelona.

"Messi na Cristiano Ronaldo. Kwa uhakika huwezi kudharau nguvu ya uchumi ya Qatar."

Neymar na PSG wanajiandaa kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich Jumapili hii, ikitoka kuifunga RB Leipzig mabao 3-0 kwenye nusu fainali.

## HABARI MICHEZO




# KAHN NA MATUMAINI ALABA KUBAKI BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

OLIVIER Kahn amesema Bayern Munich ina "matumaini" ya kumbakisha David Alaba klabuni hapo licha ya kuwaniwa kwenye Ligi Kuu ya England.

Mlinzi huyo alikuwa akihusishwa kuwaniwa na Manchester City, ambao walikuwa na nia ya kumhusisha kwenye usajili huo na dili la Leroy Sane.

Huku Sane akiwa amejiunga na Bayern na City ikitumia pauni milioni 41 kwa Nathan Ake, sasa Manchester United na Chelsea ndio wanaohusishwa na Alaba.

Hata hivyo, Kahn ana matumaini makubwa ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria kukubali kuongeza mkataba mpya mara tu ule wa sasa utakapomalizika mwaka 2021.

"Kwa sasa tunafanya mazungumzo ya mara kwa mara na David Alaba na washauri wake," alisema Kahn, ambaye anatarajiwa kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bayern mwishoni mwa mwaka huu, akiwaambia waandishi wa habari.

"Bila shaka, siwezi kuzungumzia kuhusu nini kinaendelea, lakini nafikiria tunakaribia kufikia makubaliano. Tunafanya kila tunaloweza kumbakisha David.

"Kwa wakati huu, nina matumaini tunaweza kumbakiza David."

Alaba alikuwa sehemu ya kikosi cha Bayern kilichoifunga Lyon mabao 3-0 Jumatano iliyopita na kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na



# WENGER NA SIMULIZI LA GNABRY KUONDOKA ARSENAL

**LONDON, England**

ARSENE Wenger ameelezea namna alivyosikitishwa kwamba Arsenal haikuona ubora wa Serge Gnabry.

Kwa kufunga mabao mawili katika ushindi wa 3-0 Bayern Munich iliyoupata dhidi ya Lyon Jumatano, Gnabry alifikisha mabao tisa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. Gnabry anaweza kuwa nyota kwenye fainali ya Jumapili dhidi ya Paris Saint-Germain, kwani amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia kabisa.

Aliondoka akiwa na umri wa miaka 21, Agosti mwaka 2016 na ilikuwa ni wiki chache tu baada ya kocha wa Arsenal wakati huo, Wenger kurekodiwa akisema ana matumaini Gnabry anaweza kukaa na 'Washikabunduki' hao kwa muda mrefu.

Badala yake, Gnabry alichagua kujiunga na Werder Bremen, kabla ya kwenda Bayern miezi 10 baadaye.

"Tusisahau kuhusu Gnabry, nilimnunua akiwa na umri wa miaka 15 kutoka Stuttgart na alikuwa na majeraha ya mara kwa mara," alisema Wenger akiiambia beIN Sports.

"Tulikuwa na makubaliano naye. Nilimpeleka kwa mkopo West Brom na hakucheza mchezo wowote. Alirudi tena na akawa majeruhi.

"Tulifanya naye kazi kwa muda wa miezi sita na alikwenda kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Ujerumani chini ya umri wa miaka 21, na Bayern wakafanya dili na Werder Bremen.

"Hakutaka tena kuongeza mkataba na Arsenal. Nilihuzunika sana hatukuweza kupata ubora wake, kwa sababu nilijua atakuja tu kuwa bora kwa siku za usoni."




# FATI, TRAORE WAITWA KIKOSI CHA HISPANIA

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA anayechipukia wa Barcelona, Ansu Fati ameitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania kwa ajili ya mechi za mwezi ujao dhidi ya Ujerumani na Ukraine.

Winga wa Wolves, Adama Traore ni mmoja wa wachezaji wengine ambao hawajawahi kuichezea timu hiyo akiwa amejumuishwa kwenye kikosi hicho.

Katika kikosi hicho kilichojaa damu changa nyingi chini ya kocha wake, Luis Enrique, pia kimemjumuisha mlinzi wa Manchester City, Eric Garcia na kiungo wa Real Madrid, Oscar Rodriguez, ambaye amekuwa anacheza kwa mkopo kule Leganes.

Pia upo usajili mpya wa Manchester City, Ferran Torres, pamoja na golikipa wa Athletic Bilbao, Unai Simon, kiungo wa Real Sociedad, Mikel Merino na beki wa pembeni wa Sevilla, Sergio Reguilon.

Mlinzi wa kushoto wa Barcelona, Jordi Alba ameachwa na hakuna mchezaji yeyote kutoka Atletico Madrid kwenye kikosi hicho.

Mchezo huo wa Septemba utakuwa ni wa kwanza kwa Hispania tangu mwaka jana, baada ya mechi za kimataifa kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Hispania itacheza na Ujerumani mjini Stuttgart Septemba 3, mwaka huu kabla ya kuwakaribisha Ukraine siku tatu baadaye.

Kikosi kamili: David de Gea (Manchester United), Kepa Arrizabalaga (Chelsea), Unai Simon (Athletic Bilbao); Jesus Navas (Sevilla), Dani Carvajal (Real Madrid), Sergio Ramos (Real Madrid), Pau Torres (Villarreal), Diego Llorente (Real Sociedad), Jose Gaya (Valencia), Sergio Reguilon (Sevilla), Eric Garcia (Manchester City); Fabian Ruiz (Napoli), Thiago Alcantara (Bayern Munich), Sergio Busquets (Barcelona), Rodri (Manchester City), Mikel Merino (Real Sociedad), Dani Olmo (RB Leipzig), Oscar Rodriguez (Leganes); Rodrigo Moreno (Valencia), Mikel Oyarzabal (Real Sociedad), Adama Traore (Wolves), Marco Asensio (Real Madrid), Ansu Fati (Barcelona) na Ferran Torres (Manchester City).

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# COUTINHO SASA AITULIZA ARSENAL, AGEUKIA UEFA

Akili yangu inafikiria zaidi fainali ya Ligi ya Mabingwa, kuhusu majaliwa yangu ya baadaye, sijawahi...

**LISBON, Ureno**

KIUNGO mshambuliaji wa Bayern Munich, Philippe Coutinho amesisitiza "akili yake inafikiria zaidi" fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya huku uvumi ukizidi kukua juu ya majaliwa yake.

Coutinho atacheza mechi yake ya mwisho Bayern dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye fainali ya mashindano hayo Jumapili kabla kurudi klabu yake ya Barcelona.

Hata hivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anatarajia kuondoka moja kwa moja pale Barcelona, huku Arsenal ikihusishwa kumuwania.

Lakini Coutinho, ambaye aliwasili Barcelona kutoka Liverpool Januari mwaka 2018, amesema akili yake kwa sasa inafikiria zaidi fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"AKili yangu inafikiria zaidi mashindano haya," alisema mchezaji huyo akiiambia Esporte Interativo.

"Ni nafasi ya kipekee kwa upande wetu. Nina furaha kubwa kuwa kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kuhusu majaliwa yangu ya baadaye, sijawahi kuwaza hilo kwa sasa ninachofikiria ni fainali tu."

Coutinho amefunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho tisa katika mechi 37 kwenye mashindano yote akiichezea Bayern msimu wa 2019-20.

## KWA UFUPI

**KOEMAN AMUWANIA WIJNALDUM**

KOCHA mpya wa Barcelona, Ronald Koeman, anataka kumleta kiungo wa kati wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 29 pale Nou Camp. ***(Algemeen Dagblad, via Express)***

**GABRIEL SASA HUYO UNITED**

MLINZI wa kati wa Lille na Brazil, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 22, amechelewa kufanya uamuzi wa mwisho ya kuelekea Arsenal baada ya Manchester United kuonekana kuwa na uwezekano wa kutoa kitita fulani kwa ajili yake**. *(Telegraph)***

**PSG YAMNYATIA DALOT**

KLABU ya Paris St-Germain inamnyatia beki wa Manchester United na Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 21. ***(O Jogo)***

**SMALLING ANOGEWA ROMA**

MLINZI wa kati wa Manchester United, Chris Smalling, mwenye umri wa miaka 30, anafuatilia kwa karibu makubaliano ya mkopo na AS Roma baada ya msimu uliopita kucheza kule Serie A. ***(La Gazzetta dello Sport, via Mirror)***

**HENDERSON KUFUNGWA ZAIDI**

MANCHESTER United ipo kwenye hatua ya mwisho ya mazungumzo ya kuongeza mkataba na golikipa wake, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 23. Katika mkataba huo mpya kipa huyo atalipwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. ***(Sky Sports)***

**COSTA HAENDI TENA UNITED**

KLABU ya Manchester United imeonyesha kurudi nyuma juu ya mpango wake wa makubaliano ya mkopo kwa winga wa Juventus na Mbrazil, Douglas Costa mwenye umri wa miaka 29, na badala yake inafikiria kumsajili winga wa Bournemouth na Wales, David Brooks mwenye umri wa miaka 23**. *(Manchester Evening News)***

**LIVER YAMPAMBANIA ALCANTARA**

LIVERPOOL inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich, Thiago Alcantara, huku mchezaji huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 29, thamani yake ikitajwa kuwa ni pauni milioni 30. ***(Independent)***

**DEENEY KUBAKIA WATFORD**

MSHAMBULIAJI wa Watford, Troy Deeney mwenye umri wa miaka 32, anataka kubaki hapo Hornets, licha ya timu hiyo kushushwa daraja. ***(Talksport)***

**SPURS KWA MAITLAND-NILES**

TOTTENHAM Hotspur inapanga kumsajili, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 22, kutoka Arsenal ambaye msimu uliopita alicheza kama mlinzi na kiungo wa kati kwa timu hiyo. ***(Mail)***

**VILLA YAMTAKA WATKINS**

ASTON Villa iko tayari kutoa ofa ya pauni milioni 18 kwa mshambuliaji Mwingereza wa Brentford, Ollie Watkins mwenye umri wa miaka 24, lakini upande wa mchezaji huyo unasemekana kushikilia kutaka pauni milioni 25. ***(Mail)***

**BETIS YAMTAKA MONTOYA**

KLABU ya Real Betis inafanya mazungumzo na Brighton kuhusu uhamisho wa beki wa kulia raia wa Hispania, Martin Montoya mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

# MUGALU HESABU KALI KWA BOCCO, KAGERE

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI mpya wa Simba, Chris Mugalu, amesema amekuja Tanzania kufanya kazi moja tu kucheza soka na malengo ni kupambana katika majukumu yake ili kuingia katika kikosi cha kwanza ndani ya timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mugalu alisema kwa uwezo alionao anauhakika wa kupambana kwa kutimiza majukumu yake kwenye mazoezi ili kumshawishi kocha Sven Vandenbroeck kumpa nafasi ya kucheza.

Alisema hakuna njia mbadala ya kucheza kikosi cha kwanza, zaidi ya kuhakikisha anajituma katika mazoezi ili kumshawishi kocha kumpa nafasi.

"Lazima nipambane katika mazoezi ili nimshawishi mwalimu kunipa nafasi katika kikosi cha kwanza, itakuwa ngumu kuingia moja kwa moja kwa sababu tayari kuna mtu nimemkuta, hivyo natakiwa kujituma zaidi ili nipate nafasi ya kuingia katika mfumo wa kocha haraka," alisema Mugalu ambaye ni raia wa DR Congo.

Alisema hakuna urahisi wowote kwa mchezaji mpya kupata nafasi moja kwa moja kwa kuwa kuna watu ambao tayari wameshajihakikishia nafasi na kocha kuwaamini.

"Kwa yeyote yule anapokwenda katika timu mpya unatakiwa kuonyesha kiwango kizuri ili kuwa bora zaidi ya wenzako uliowakuta, malengo yangu ni kupambana ili kupata nafasi katika kikosi cha kwanza," alisema mshambuliaji huyo aliyejiunga na Simba katika dirisha hili la usajili akitokea Lusaka Dynamos ya Zambia.

Aidha, alisema hakuja kuwaangusha viongozi na mashabiki wa timu hiyo na kwamba kilichomleta ni kushirikiana na wenzake aliowakuta kwa ajili ya kuipa Simba mataji na kucheza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mugalu ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia Simba sambamba na kiungo Larry Bwalya ambaye naye anatokea Lusaka Dynamos, atakuwa na jukumu la kuwania namba katika safu ya ushambuliaji dhidi ya mzawa John Bocco na Mnyarwanda Meddie Kagere.

# Ndondo Cup sasa mubashara Plus TV ndani ya DStv

**Na Mwandishi Wetu**

MICHUANO ya soka nchini maarufu kama Ndondo Cup ambayo tayari imeanza kutimua vumbi jijini Dar es Salaam ikishirikisha timu 34, imechukua sura mpya baada ya benki ya KCB kutangaza kudhamini mashindano hayo huku ikionyeshwa mubashara kupitia PlusTV ndani ya Kisimbuzi cha DStv.

Akizungumza jana wakati wa kutangaza udhamini huo ambapo benki hiyo imetoa Sh. milioni 50, Mkurugenzi Mtendaji wa KCB, Cosmas Kimario, alisema wameamua kudhamini mashindano hayo kwa kuwa yamekuwa ni chimbuko la vipaji vya wanasoka vijana hapa nchini na kwamba mafanikio yanayopatikana katika michuano hiyo ndiyo yaliyowavutia kuamua kuidhamini.

"Tumeona jinsi ambavyo mashindano hayo yalivyo mbali na kuwa burudani kwa wakazi wa Dar es Salaam, lakini pia yamekuwa chimbuko la wachezaji wenye vipaji. Kwa hiyo tumeona tukishirikiana na waandaaji, tunaweza kuyafanya mashindano haya kuwa makubwa na bora zaidi na hivyo kuleta faida kubwa kwa soka la Tanzania," alisema Kimario.

Mkurugenzi huyo amebainisha kuwa KCB Bank imekuwa mbia muhimu katika michezo hapa nchini na wanatarajia kuwekeza zaidi ili kuongeza mchango wao kwa maendeleo ya jamii.

"Mbali na biashara yetu ya msingi ambayo ni kutoa huduma bora za benki kwa Watanzania, pia tumewekeza sana kwenye miradi ya kijamii ikiwemo kukuza michezo hapa nchini, ambapo pia sisi ni wadhamini wenza wa Ligi Kuu Tanzania Bara".

Huu ukiwa ni mwaka wa saba tangu kuanza kwa mashindano hayo yanayoandaliwa na Clouds Media Group, tayari Ndondo Cup imekuwa na mafanikio makubwa ikiwemo kutoa wachezaji zaidi ya 100 ambao wameingia mikataba na klabu mbalimbali za ndani na nje ya nchi ikiwamo Ligi Kuu.

Mratibu wa michuano hiyo, Shafi Dauda alisema kutokana na udhamini huo wa KCB na kwa kuwa michuano hiyo sasa inaonekana mubashara kupitia PlusTV ndani ya Kisimbuzi cha DStv, bila shaka umaarufu wa mashindano hayo utaongezeka kwani sasa yataonekana hadi nje ya nchi ambapo DStv inaonekana.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB, Cosmas Kimario (kushoto), Mratibu wa Mashindano ya Ndondo Cup, Shaffi Dauda (katikati) na Mkuu wa Plus TV, Ramadhani Bukini (wa tatu kulia) wakionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 50, walizokabidhiwa waandaji wa Ndondo Cup jijini Dar es Salaam jana kutoka kwa wadhamini wa michuano hiyo, KCB. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania – DStv, Jacqueline Woiso, ambaye ameridhia michuano hiyo kuonyeshwa mubashara kupitia Plus TV ndani ya DStv. **MPIGAPICHA WETU**

"Kwa kweli udhamini huu wa KCB Bank pamoja na kuonyeshwa michuano hii mubashara kwenye DStv kupitia PlusTV kutayafanya yaonekane kwenye nchi mbalimbali hivyo kuongeza wigo wa wachezaji wetu kuonekana na kuongeza uwezekano wa wachezaji kupata fursa za kuchukuliwa na klabu kubwa ndani na nje ya nchi, alisema Dauda.

Dauda alisema bingwa wa michuano hiyo ambayo imeanza kwa kuchezwa kwa mfumo wa makundi, mbali na kombe pia atajinyakulia kitita cha Sh. milioni 10, mshindi wa pili akiibuka na Sh. milioni tano, wa tatu Sh. milioni tatu na wanne Sh. milioni mbili.

"Kadhalika kutakuwa na zawadi kwa mchezaji bora, kipa bora na mwamuzi bora kila mmoja atazawadiwa Sh. 500,000 huku kikundi bora cha ushangiliaji kikiibuka na Sh. milioni moja na shabiki bora laki mbili," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa PlusTV, Ramadhani Bukini, alisema wamejipanga vizuri kuwapa Watanzania na Ulimwengu kwa ujumla burudani ya Ndondo Cup. "Tunaona fahari kubwa sana kuwa wabia wa mashindano haya na kama mnavyojua, Plus TV tunaonekana katika mataifa mengi ya Afrika kupitia DStv hivyo tunawapa fursa wapenda soka kushuhudia michuano hii mubashara," alisema Ramadhani.

Alisema Ndondo Cup itaonekana katika nchi 36 za Afrika zikiwamo, Ghana, Cameroon, Nigeria, Equatorial Guinea, Kenya, Uganda, Cape Verde, Angola, Guinea na kwingineko.

Mkurugenzi Mtendaji wa wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso yeye alisema kwa muda mrefu mashindano ya hapa nchini yamekuwa hayaonekani nchi za nje kitendo ambacho kinazorotesha ukuaji wa michezo hapa nchini.

"Tunafahamu wazi kuwa wachezaji wakiwa uwanjani ni sawa na kuwa sokoni kuuza uwezo na vipaji vyao, sasa kama michezo hiyo haionekani kimataifa, watu wa nje wataonaje na kujua uwezo wa wachezaji wetu? Alihoji huku akiwataka Watanzania kujivunia michuano hiyo kuonekana kupitia PlusTV ndani ya DStv.

## Usajili Ligi Bara wapamba moto

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikibaki wiki moja tu kukamilika kwa usajili wa wachezaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, klabu zinaendelea kupigana vikumbo kuwania saini za wachezaji mbalimbali ndani na nje ya nchi, huku klabu za Biashara United, Mtibwa Sugar na Ihefu FC zikiamka kutoka kwenye usingizi mzito na 'kushusha vifaa vya hatari.'

**Klabu ya Biashara United imewasajili wachezaji wawili raia wa Uganda, golikipa Ssetuba James na Zziwa Joseph.**

Klabu ya Ihefu FC nayo baada ya kimya tangu ilipopanda Ligi Kuu, imemsajili straika wa Mbao FC, Jordan John, na Wema Sadoki aliyekuwa Alliance FC.

Klabu ya Mtibwa Sugar ambayo nayo ilikuwa kimya, imeibuka na kumsajili kwa mkopo straika wa Azam, Abal Kassim Hamisi ambaye pia huichezea timu ya Zanzibar Heroes, lakini vile vile imemsainisha kiungo ambaye alikuwa akiwaniwa na klabu kubwa za Simba, Yanga na Azam, Baraka Majogolo, mchezaji aliyefanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika.

Klabu ya Namungo FC yenyewe imeendeleza kujiimarisha kwa kusajili wachezaji kadhaa na jana kwenye mtandao wake rasmi ilimtambulisha beki wa kati kutoka Kariobangi Sharks ya Kenya, Amani Pter Kyata.

## Tenesi watoto sasa Gymkhana Arusha

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi ya mchezo wa Tenesi kwa watoto wenye umri kuanzia miaka 5-12 yatafanyika Septemba 12-13, mwaka huu, katika Klabu ya Gymkhana jijini Arusha yakiwa na lengo la kupata wachezaji watakaounda timu ya Taifa.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Mwenyekiti wa Chama cha makocha katika Klabu ya Gymkhana jijini Dar es Salaam, Rajabu Borry, alisema wanaendelea kuwanoa wachezaji wao kuelekea katika mtanange huo.


"Tunaendelea vizuri na mazoezi kwa lengo la kuwaweka sawa watoto ambao wanajiandaa na mashindano hayo, kikubwa tunaomba sapoti kutoka kwa wadau mbalimbali ili tufanikishe malengo yetu," alisema Rajabu.

Alisema kipindi kilichopita walishindwa kufanya mashindano mbalimbali kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

# Michezo

Jumamosi Agosti 22, 2020

Nipashe

## Coutinho sasa aituliza Arsenal, ageukia UEFA

HABARI UK 22

**MAJEMBE YA KAZI...**




Nyota wapya wa Simba, kutoka kushoto Larry Bwalya, Chris Mugalu na Bernard Morrison (kulia) wakiwa mazoezini na kiungo mkongwe wa klabu hiyo, Jonas Mkude (wa pili kulia). Wachezaji hao watashuka Uwanja wa Mkapa leo kuivaa Vital'O ya Burundi kwenye mechi ya Simba Day. **PICHA: SIMBA**

# NI WEKUNDU DAY

### ●●● Wapya wote kucheza leo, Mo amuonya Morrison, Sven naye apewa mtihani mzito...

**Na Saada Akida**

NI Wekundu Day! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema, baada ya siku ya kilele cha mabingwa wa soka nchini Simba 'Wekundu wa Msimbazi' maarufu kama Simba Day kutimia huku tamasha kubwa likifanyika leo katika viwanja viwili, Uwanja wa Mkapa na wa Uhuru.

Tangu juzi mashabiki wa soka nchini hususan wa Simba wamekuwa wakijazana katika vituo vya kuuzia tiketi kuzinunua tayari kwa kuhudhuria tamasha hilo la 'Siku ya Wekundu', ambalo linatarajiwa kutawaliwa na burudani ikiongozwa na msanii 'baba wa muziki' nchini pengine hata Afrika kwa sasa, Diamond Platinumz.

Kila kona nchini hususan Dar es Salaam, huwezi kupishana na watu zaidi ya 10 bila kukutana na aliyevaa jezi nyekundu ya Simba na kwa namna misururu ya kununua tiketi ilivyokuwa mirefu tangu juzi, ni wazi Uwanja wa Mkapa na Uhuru vinaweza kutapika leo.

Kwa mujibu wa uongozi wa Simba, watakaoingia katika Uwanja wa Uhuru watashuhudia tamasha hilo mubashara kupitia televisheni wakati shughuli zote zikiendelea dimba la Mkapa.

Simba itatumia tamasha hilo kutambulisha jezi mpya za msimu, kikosi chao cha 2020/21 pamoja na kuuza vifaa mbalimbali vya michezo vya klabu hiyo, lakini pia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Vital'O ya Burundi.

Katika hatua nyingine, Sven alisema wachezaji wote waliosajiliwa ambao tayari wameanza mazoezi leo watapewa nafasi ya kucheza dhidi ya Vital'O.

Na kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugezi wa Simba, Mohamed "Mo" Dewji, amesema tayari wamempa mtihani mzito, Kocha wao Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck kuhakikisha yeye na benchi lake la ufundi wanafikia shabaha yao ya kucheza hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika.

Aidha, Mo amesema amempigia simu kiungo mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Mghana Bernard Morrison aliyesajiliwa na klabu hiyo baada ya kumaliza mkataba na Yanga, na kumuonya kwa kumtaka abadilike kinidhamu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana katika ofisi zake, Mo alisema baada ya kumalizika msimu huu, alikutana na Sven na kumpa masharti ya kuhakikisha wanatetea taji la ubingwa pia kufikia hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema wana imani na kocha huyo kufikia malengo yao, lakini wanataka kuweka mambo mazuri katika suala la nidhamu na kukomesha wachezaji wavivu katika timu yetu.

"Sven amefanikiwa kwa Tanzania, anaelewa kwamba shabaha yetu ni kufika hatua ya makundi, hivyo ana kazi kufikia tunachokihitaji, ila hatuwezi kufika hapa lazima tuwe na wachezaji wenye nidhamu.

"Tunatambua kwamba Bernard Morrison amekuwa mtovu wa nidhamu katika timu aliyotoka, hivyo baada ya kusaini mkataba na kuwa mali yetu, nilimpigia simu na kumuonya kuhusu nidhamu yake," alisema Mo.

Alisema lakini wamesisitiza kwa wachezaji wavivu kwa kuleta kifaa maalum (GPS) kwa ajili ya kuwapima wakati wa mazoezi.

"Huwezi kupata mafanikio kwa wachezaji wenye nidhamu mbovu, tayari tumelifanyia kazi, lakini kuanzia wiki ijayo, Jumanne, tutawakomesha wavivu kwa kifaa hicho kuanza kutumika rasmi," alisema Mo Dewji.

# SENZO: SABABU KUJIUZULU SIMBA HII

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa, ameweka wazi sababu ya kujiuzulu nafasi hiyo kabla ya kuamua kujiunga na Yanga, huku akiwaomba radhi mashabiki wa klabu hiyo kwa kuwataka kukubaliana na kilichotokea kwa sababu pamoja na yote mpira kwake ni kazi na ndio unaoendesha maisha yake.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mara baada ya kurejea akitokea kwao Afrika Kusini, Senzo alisema anafahamu kwa namna moja au nyingine kuachana kwake na Simba huku akijiunga na Yanga ni uamuzi ambao umewaumiza mashabiki wa timu hiyo.

Alisema: "Mambo ambayo yalinifanya kuchukua uamuzi wa kuondoka ni pamoja na kukosa furaha, kama huna furaha namna nzuri ya kufanya ni kuondoka, sikuondoka kwa ubaya ndio maana niliwatakia kila la kheri, hivyo mashabiki wanisamehe kwa sababu kilichotokea ni sehemu ya maisha kwangu mpira ni kazi, unaendesha maisha yangu."

Kadhalika, Senzo alisema suala lingine lililomfanya kuondoka ni kutokana na mtazamo na kwamba wakati akifanya uamuzi huo hakuwa na lengo la kwenda kujiunga na Yanga.

Huku akiitakia mema klabu ya Simba katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayoshiriki, Mazingisa alisema sasa anachukua jukumu jipya kwenye klabu yangu ya Yanga kwa kuisaidia katika suala zima la namna ya uendeshaji.

Kuhusu kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, raia wa Msumbiji, Luis Miquissone ambaye anadaiwa kutokuwa na mkataba halali na klabu hiyo, Senzo alisema: "Ana mkataba wa miaka mitatu na nusu kuitumikia Simba.

"Ilikuwa shughuli kumpata Luis ila sitazungumzia kuhusu klabu yangu ya zamani, nazungumza mimi kama niliyehusika kumleta, nasema ni mchezaji wa Simba kwa miaka mitatu na nusu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >